SportPesa
TZS. 1,065,872,000
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Mrema** ataja sababu kuoa mke mwingine

UKURASA 3




**CAVANI KWENDA KUVAA VIATU VYA SANCHEZ INTER**

UKURASA 21

Nipashe
Jumatano Machi 23, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580893
www.ippmedia.com
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Wapendekeza mambo 12 siasa, demokrasia

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan akifungua pazia kuzindua mradi wa maji wa Mlandizi-Chalinze-Mboga, Chalinze, mkoani Pwani jana. Wengine ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (wa nne kushoto), Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete (wa tatu kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja (kushoto) na (wa pili kulia) ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### ULAYA YAIPATIA TANZANIA BIL. 469/-

UMOJA wa Ulaya (EU) umeipatia Tanzania msaada wa Euro milioni 180 (Sh. bilioni 469) kwa ajili ya ufadhili wa miradi mitatu, ukiwamo wa kuboresha masuala ya...

UKURASA WA 4

### MELI KUBWA YA UVUVI KULETA FURSA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema Tanzania itanufaika kwa kuingiza shilingi bilioni moja kila mwaka na tani 300 za samaki, baada ya...

UKURASA WA 5

### MBARONI DAR MADAI UPORAJI FEDHA BENKI

JESHI la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam linawashikilia watuhumiwa wawili wa ujambazi wanaodaiwa kujihusisha na vitendo vya kuwafuatilia na kuwapora...

## Rais aonya upandishaji holela wa bei vifaa vya maji

UKURASA 3



## Operesheni ‘sakasaka’ wasio na vibali vya uhamiaji yaja nchini

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA: SUBIRINI MTAFURAHI TU UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana, kuhusu mapendekezo ya kituo hicho, kwa kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi nchini. Kulia ni Ofisa Programu, Wanawake na Watoto wa kituo hicho, Getrude Dyabene. **PICHA: SABATO KASIKA**

# LHRC, wadau wapendekeza mambo 12 vyama vya siasa

**Na Waandishi Wetu**

WADAU wa siasa wametoa maoni kuhusu uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kuridhia pendekezo la kikosi kazi cha kuratibu demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Miongoni mwa mambo hayo ni matokeo ya urais kupingwa mahakamani.

Wadau hao ni Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ambacho kimetoa mapendekezo 12 ikiwamo kuruhusu matokeo ya urais kupingwa mahakamani iwapo kutakuwa na malalamiko ya msingi na kuruhusu mgombea binafsi, kwa ajili ya kuimarisha demokrasia ya vyama vya siasa nchini.

Mapendekezo hayo, yalitolewa Dar es Salaam jana na Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo ya kipaumbele ya LHRC.

Alisema, wamefuatilia uwasilishwaji wa ripoti ya Kikosi Kazi hicho kwa Rais Samia Suluhu Hassan, na kuamua kutoa mapendekezo ambayo kikosi hicho ni vyema kikayazingatia wakati wa ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau.

"Tunapendekeza kuruhusu matokeo ya kiti cha urais kupingwa mahakamani ikiwa kuna malalamiko ya msingi, kwani tunachukulia kama ilivyoamuliwa na Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu katika kesi ya Jebra Kambole dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Na. 018/2018," alisema Henga.

Alifafanua kuwa, mahakama hiyo iliamua kuwa Ibara ya 41 (7) ya kutopinga matokeo ya urais ni kinyume cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981.

Kuhusu suala la mgombea binafsi, alisema hatua hiyo itakwenda sawa na uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, katika kesi ya Mchungaji Christopher Mtikila dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Na. 011/2011.

"Hatua hiyo ya kuwapo kwa mgombea binafsi, itasaidia kupunguza urasimu wa vyama vya siasa ambavyo hutumia sifa za uanachama dhidi ya wagombea, ikitokea kutoelewana kati ya pande mbili," alisema.

Alisema, LHRC pia inapendekeza kuwapo mfumo wa 50+1 kuwa kigezo cha ushindi wa uchaguzi mkuu, na kuwe na uwakilishi sawa wa jinsia wa 50/50 kwa kuweka kipengele mahsusi kitakachoweka sharti kwa sera au sheria yoyote kuzingatia usawa wa kijinsia.

Mapendekezo mengine ni Jeshi la Polisi kutoingilia shughuli za vyama vya siasa wakati, kabla na baada ya kampeni kinyume cha sheria, na kushauri tume ya uchaguzi kuwa na watumishi wake, ili wakurugenzi wa halmashauri wasiwe wasimamizi wa uchaguzi katika ngazi ya jimbo.

"Lakini pia mkurugenzi wa uchaguzi, mwenyekiti wa tume ya uchaguzi na makamishna wapatikane kwa kuomba kazi ambazo zinatangazwa hadharani na uteuzi wa wajumbe wa tume ya uchaguzi uzingatie uwakilishi wa vyama vikubwa vya siasa, asasi za kiraia, taasisi za kidini na wanataaluma," alisema.

Henga alisema, LHRC inashauri kigezo cha kupita bila kupingwa kiondolewe, hata kama mtu atapita bila kupingwa kuwe na kura ya ndiyo au hapana, na pia kuwe na mfumo wa kielektroniki wa kupiga kura.

Aidha, kuwe na takwa la kisheria kwa vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia na watu wenye ulemavu wakati wa mchakato wa uteuzi.

"Mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa ifanyike kwa usawa kwa vyama vyote, na pia nafasi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iwe ya kutangazwa hadharani kwa vigezo vitakavyoanishwa na kamati maalum ya kuajiri,"alisema.

Pia, Sheria ya Vyama vya Siasa ifanyiwe marekebisho na kuondoa yale yaliyofanyika mwaka 2019 ambayo kwa kiasi kikubwa yalirudisha nyuma ustawi wa demokrasia ya vyama vingi.

**WADAU WENGINE**

Mhadhiri wa Chuo Kikuu Huria, Dk. Albert Memba, alisema uamuzi wa Rais Samia kuridhia pendekezo la kikosi kazi cha kuratibu demokrasia ya vyama vingi vya siasa la kutaka kuwapo kwa tume huru ya uchaguzi

unaonyesha kuwa serikali inakusudia kujenga jamii yenye haki na usawa wa ushiriki kwenye vyombo vya uamuzi na vyama vya siasa.

"Hakuna ubaya wowote kwenye kutengeneza tume huru au katiba mpya, isipokuwa tu anaangalia ikae katika mpango wa sasa, wa kati au wa muda mrefu, lakini pia kipi kipewe kipaumbele, kwa hiyo hatua aliyoichukua ni ya mtu mwenye maono mapana kuhusu mwelekeo wa nchi yetu," alisema.

Dk. Memba alisema anaimani pia timu iliyoundwa kufanya kazi ya kukusanya mapendekezo ikiongozwa na Prof. Rwekaza Mukandala itafanya kazi nzuri kwa sababu ni watu wabobezi waliofanya kazi katika taasisi za uchambuzi na utafiti wa masuala ya kidemokrasia kwa muda mrefu.

Mchambuzi wa masuala ya siasa, Prof. Ernest Mallya, alisema tume huru inatakiwa iendane na uadilifu na teknolojia inayoweza kuzuia ubadhirifu unaofanyika katika mchakato wa uchaguzi.

Naye Mhadhiri kutoka Chuo cha Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia Dar es Salaam, Godwin Gonde, alisema Watanzania wanapaswa kuwa na subira, kwa kuwa kila upande umepewa ahadi.

Gonde alisema mchakato wa katiba mpya una gharama kubwa, ikiwamo fedha, si jambo la kuharakisha, kwamba inawezekana kikosi kazi hicho kiliangalia yote na kutoa mapendekezo.

Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, alisema kutangulia kwa katiba mpya ndilo jambo la msingi, kwa kuwa ndiyo mama wa tume huru ya Uchaguzi na ndiyo yenye uwezo wa kutatua changamoto za kiuchumi, kijamii na kisiasa zinazolikabili Taifa.

**Imeandikwa na Sabato Kasika na Jenifer Gilla**

# Operesheni 'Sakasaka' wasio na vibali uhamiaji yaja rasmi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

KAMISHNA Jenerali wa Jeshi la Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, ametangaza wiki moja ya operesheni maalumu nchi nzima ya kuwasaka watu walioingia nchini bila kibali.

Amesema operesheni hiyo iliyopewa jina la 'Sakasaka' pia italenga kukagua uhalali wa wageni waliopo nchini ili kujiridhisha kama wamekidhi vigezo na masharti.

Aliyasema hayo jana baada ya kuwasili mkoani Morogoro na kukagua karakana ya uhamiaji mkoa na kupata taarifa namna walivyojipanga kutekeleza operesheni hiyo maalumu ya siku saba.

Dk. Makakala pia alionya tabia ya baadhi ya Watanzania kuendelea kutumia wahamiaji haramu kama sehemu ya kujipatia kipato, kwa kuwa wamekuwa ndiyo chanzo cha raia wa kigeni kuingia nchini bila kibali.

Kadhalika, Dk. Makakala alibainisha chanzo cha ongezeko la wahamiaji haramu kuwa ni baadhi ya wananchi wasio wazalendo.

Hata hivyo, alisema wameendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na wananchi na vyombo vingine vya usalama na kuwatahadharisha wanaotaka kujihusisha na biashara ya usafirishaji haramu kuacha mara moja ili kuepukana na adhabu zinazotolewa.

Kadhalika, Dk. Makakala alizungumzia mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani hasa kwa kuangazia jeshi hilo kwa kuongeza askari.

"Morogoro inafanya vizuri kwa kuongoza kukamata wahamiaji haramu wanaoingia nchini ndiyo maana hata katika kuongeza nguvu, tutaiangalia Morogoro kipekee," alisema Dk. Makakala.

Alisema wamepata ajira za vijana takribani 820 ambao watakwenda kuongeza nguvu katika mikoa yote hasa ambayo wahamiaji haramu wamekuwa wakikamatwa mara kwa mara ikiwamo Morogoro.

"Katika kudhibiti wahamiaji hawa haramu kutoka Ethiopia ambao wamekuwa wakikwama kuendelea na safari zao na wengine kuishia katika vifungo magerezani, tumekuja na mfumo wa Viza rejea ambao utatoa uelekeo wa namna ya kupambana na usumbufu unaojitokeza wa matumizi ya njia za panya," alisema.

Vile vile, alisema Jeshi la Uhamiaji limekuwa na mchango katika ukuaji wa uchumi kutokana na wawekezaji na wafanyabiashara wa kigeni kuendelea kuongezeka nchini.

Aidha, alisema taratibu za upatikanaji wa vibali vya uwekezaji na biashara sasa huchukua siku chache kukamilika.

## EU yaipatia Tanzania bil. 469/-

**Na Gwamaka Alipipi**

UMOJA wa Ulaya (EU) umeipatia Tanzania msaada wa Euro milioni 180 (Sh. bilioni 469) kwa ajili ya ufadhili wa miradi mitatu, ukiwamo wa kuboresha masuala ya kijinsia.

Hafla ya utiaji saini mikataba hiyo ilifanyika jana jijini Dar es Salaam kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba na Balozi wa EU Tanzania, Manifredo Fanti.

Akizungumza baada ya hafla hiyo, Tutuba alisema mikataba hiyo ni sehemu ya Euro milioni 703 ambazo EU imetenga kuisaidia Tanzania chini ya mpango wa miaka saba wa ushirikiano kuanzia mwaka 2021 hadi 2027. “Mradi wa kwanza ni wa kuboresha masuala ya kijinsia wenye thamani ya Euro milioni 70, wa pili ni mradi wa kuwa na miji ya kijani wenye thamani ya Euro milioni 75. Mradi wa tatu ni wa kidijitali wa serikali mtandao wenye thamani ya Euro milioni 35,” alisema Tutuba.

Alisema mradi wa kuboresha masuala ya kijinsia utafanikisha kuimarisha uhuru na kuondoa aina zote za ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma na binafsi, shuleni, mahali pa kazi na mitandaoni kwa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana.

Pia alisema mradi huo utawawezesha wanawake kiuchumi, ikijumuisha na fursa endelevu za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), pamoja na kuimarisha usawa katika uongozi na maamuzi, ikijumuisha masuala ya haki, amani na usalama. Alisema mradi wa kuwa na miji ya kijani na janja utaimarisha mazingira wezeshi maeneo ya mijini na kuimarisha upatikanaji wa mapato ya ndani na maendeleo jumuishi ya uchumi katika maeneo ya mijini. Tutuba alisema pia itaimarisha huduma za umma kwa jamii maskini maeneo ya mijini, hasa katika makazi ya majiji ya Mwanza na Tanga na kisiwa cha Pemba pamoja na kuchochea uchumi endelevu katika miji iliyochaguliwa, kwa kutengeneza fursa za kiuchumi hasa kwa wanawake na vijana. Kuhusu mradi wa kidijitali wa serikali mtandao, Tutuba alisema utawezesha uboreshaji wa uchumi wa TEHAMA na huduma za mitandao serikalini, kuongeza huduma za mitandao ya mawasiliano zinazofikika kwa usawa katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji, hususani kwenye huduma za kijamii pamoja na kuendeleza sekta ya Teknolojia ya huduma za kifedha na uvumbuzi nchini na kikanda.

Balozi Fanti alisema ushirikiano kati ya EU na Tanzania ni wa zaidi ya miaka 46, kwamba umekuwa kwenye sekta mbalimbali ikiwamo barabara, afya, elimu, tafiti.

# Rais Samia aonya upandaji holela bei za vifaa vya maji

**Na Waandishi Wetu**



RAIS Samia Suluhu Hassan, ameonya upandaji holela wa bei za vifaa vya maji hatua ambayo inasababisha miradi mingi kukwama na kuwakosesha wananchi huduma hiyo muhimu.

Akizungumza wakati wa kilele cha Wiki ya Maji, Dar es Salaam jana, Rais Samia alisema anashangaa kuona vifaa vinavyotoka nje bei zake ni nafuu kulinganisha na vile vinavyotengenezwa nchini.

“Baada ya kuona hali hiyo, tumefanya uchunguzi kinachosababisha hali hiyo na tukagundua kuwa mainjinia (wahandisi) wanawake ongezeko la asilimia 10. Naomba tabia hii iachwe mara moja,” alisema.

Pamoja na kuonya tabia hiyo, Rais alielezea kuridhishwa na kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji maeneo mbalimbali nchini huku akibainisha kwam kwa sasa hali ya upatikanaji wa maji mijini ni wastani wa asilimia 86 na vijijini ni asilimia 72.3. alisema hatua hiyo inatia moyo na inaonyesha mwelekeo mzuri.

Rais alisema siri ya yote hayo ni utendaji mzuri katika wizara na taasisi zake zikiwamo mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

“Ndiyo maana hata katika mageuzi ya Januari (mabadiliko katika Baraza la Mawaziri) Wizara ya Maji sikuigusa kabisa kwa sababu ya utendaji wao. Hata huyu (Juma) Aweso (Waziri wa Maji) hajanizingua ndiyo maana hatujazinguana,” alisema.

Rais Samia pia alizindua mifumo miwili ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) inayowezesha ufuatiliaji wa miradi ya maji pamoja na ulipaji wa bili za maji. Mifumo hiyo, alisema itasaidia kuongeza ufanisi wa shughuli za wizara hiyo na ufuatiliaji wa kina wa miradi ya maji pamoja na kuwa mwarobaini wa malalamiko ya wananchi kubambikiwa bili za maji.

Akielezea mifumo hiyo jana mbele ya Rais, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Antony Sanga, alisema wameianzisha ili kuongeza ufuatiliaji wa miradi na utoaji wa huduma za maji.

Sanga alisema kuwa wataalamu wa ndani wametengenza Maji App ambayo itaonyesha miradi yote nchini.

“Katika mkoa anaweza kuwa mkuu wa mkoa au wilaya au mwananchi wa kawaida atajisajili na kujua katika mkoa wake au wilaya aliopo ni mradi gani unatekelezwa,” alisema Sanga.

**BWAWA LA KIDUNDA**

Rais Samia Suluhu Hassan, amesema serikali itaendelea na ujenzi wa Bwawa la Maji la Kidunda na Rufiji licha ya kwamba gharama zake ni kubwa na utachukua miaka mitatu.

Alisema bwawa hilo litatumika kwa matumizi ya shughuli za binadamu na kusaidia kumaliza changamoto ya kukosekana kwa maji mkoani Dar es Salaam.

Pia alisema mradi wa miji 28, itatekelezwa kikamilifu kama ilivyopangwa na kwamba miradi 24 itatekelezwa kwa fedha za udhamini na minne kwa fedha za ndani.

“Maji hayana mbadala ni rasilimali inaweza kuisha endapo haitahifadhiwa, hivyo Watanzania watunze mazingira ili kupunguza kumaliza vyanzo vya maji nchini,” alisema Rais Samia.

Kuhusu kasi ya usambazaji maji, Rais Samia alisema, bado haijafika kwa wananchi hivyo mamlaka za maji ziendele kusambaza huduma hiyo kwa sababu ndilo lengo la wizara hiyo na watapata fedha na kuendelea kupanua huduma hizo.

**Imeandikwa na Frank Monyo na Mary Geofrey**

# Mrema ataja sababu za kuoa tena

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), Agustino Mrema, ameeleza sababu iliyomsukuma kuoa kuwa ni kuishi maisha matakatifu na kuondokana na matamanio na kuzini kwa macho.

Mrema alisema hayo juzi kijijini kwao Kiraracha, Moshi mkoani Kilimanjaro wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ndoa yake baada ya kuwapo kwa taarifa mbalimbali katika mitandao ya kijamii kuhusu yeye kuoa.

“Ukiangalia afya yangu si kwamba sina vijana wa kazi. Wapo wawili lakini kuna nafasi ya mwanamke. Amri ya tisa inasema usitamani mwanamke asiye mke wako. Huwezi kuwa na mwanamke anakusafisha, anakuogesha, anafua nguo zako, kwa matamanio ya kibinadamu utamtamani.

“Ni kosa na ni dhambi, kuliko kumtamani kwa macho afadhali umchukue kihalali. Nimefuata taratibu zote za kanisa ninataka nikifa nizikwe vizuri nisizikwe kama mbwa, labda baada ya mke kufa alikuwa mzinzi, changudoa.

“Ninataka kuishi maisha matakatifu ndiyo maana nikaenda kwa wazazi wake na wakaridhika, tukaenda kwa Paroko wa kwake akakubali na kwa Paroko wangu nikakubaliwa, ninaendelea na mafundisho, tutafunga ndoa tarehe 24 (Machi mwaka huu),” alisema.

Mrema alifafanua kuwa uzee ni namba na si sababu ya mtu kuishi maisha ya upweke.

“Unaweza ukawa na wafanyakazi wakakufanyia kila kitu lakini mke ana nafasi yake. Kwenye mtandao wameandika ‘Mrema anapingwa na watoto, watoto hawataki aoe’. Wanawasingizia watoto wangu, nina baraka zao zote,” alisema.

Alibainisha kuwa watoto wanaweza kupeleka chakula lakini huduma zingine hawawezi kumpelekea.

“Kusema napingwa, sioni mtoto aliyenipinga. Watoto wangu wanaishi vizuri, sina mpinzani, wala waumini ninaosali nao. Ndoa imetangazwa wiki tatu kanisani kama sheria inavyotaka.

Alisema alikuwa na mke ambaye alimtunza vizuri lakini Mungu akamchukua, hivyo hawezi kukaa peke yake.

“Hakutakuwa na matarumbeta ya kushangilia, washangilie nini? Lionekane ni tukio la kawaida. Ni bahati mbaya nimelazimika kuwa na mwenza baada ya mwenzangu kufariki (dunia). Nimekuwa mpweke, ninahitaji mtu wa kunitunza, kunihudumia,” alisema.

Mrema alisema kichwa cha habari ndicho kilichowapeleka waandishi wa habari nyumbani kwake kumhoji.

“Kuona Mrema anaoa dogodogo, mwanamke mweupe, kuoa ni takwa la Biblia. Kama ulioa mke wako amekufa, sheria za kanisa zinaruhusu kama una uwezo na unajisikia. Kuoa si dhambi na si kosa. Unatafuta mwenza ambaye atakufanyia tathmini akiridhika na wewe anatumikia maisha yake kukusaidia,” alibainisha.


**EAGLE RECOVERIES LIMITED**

**TANGAZO LA NOTISI/MNADA**

KWA NIABA YA **NCBA BANK TANZANIA LIMITED WA S.L.P 20268, DAR ES SALAAM.** TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA MDAIWA ALIYETAJWA HAPO CHINI ALIPE DENI LAKE ANALODAIWA KWA MUDA MREFU , ENDAPO ATASHINDWA KULIPA KWA MUDA ULIOTOLEWA DHAMANA YAKE ITAUZWA KWA RATIBA IFUATAYO.

| NA. | JINA LA MDAIWA | MALI INAYOUZWA | MAHALI ILIPO MALI INAYOUZWA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | **NG’OSHANDIMU ENTERPRISES. LIMITED/ DOTTO KILEKA NG’WANGU** | NYUMBA YENYE HATI CT.37565, KIWANJA NA.194, KITALU NA.” T” YENYE UKUBWA WA SQM 525 | ENEO LA ISANDULA, WILAYA YA MAGU, MWANZA (NYUMBA HII INAPAKANA NA KISALE LODGE NA NI MITA CHACHE KUTOKA NGUDU ROAD, | JUMATANO 06/04/2022 KUANZIA SAA 5 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mnada utafanyika sehemu ilipo dhamana.
3. Mnunuzi atakayefika bei ya juu atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei iliyofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya mnada
4. Endapo mteja atashindwa kumaliza 75% ndani ya siku 14 kiasi kilichotolewa awali 25% hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
5. Gharama za kubadilisha hati miliki (Transfer of ownsership) pamoja na gharama nyingine ni juu ya mnunuzi.

**Wote mnakaribishwa.**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**

**EAGLE RECOVERIES LIMITED,**
S.L.P 34462,
DAR ES SALAAM,
SIMU NA.0753 351 588/ 07683 152 822 /0743448888
EMAIL: eaglerecoveries2017@gmail.com

**MKURUGENZI MTENDAJI,**

**NCBA BANK TANZANIA LIMITED,**
SS.L.P 20268,
AMANI PLACE,OHIO STREET
DAR ES SALAAM.
SIMU NA. +255 22 2125710
EMAIL: info@ncba.co.tz
WEB: www.ncbagroup.co.tz

HABARI KITAIFA

# Meli kubwa ya uvuvi kuleta fursa

**Na Moshi Lusonzo**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema Tanzania itanufaika kwa kuingiza shilingi bilioni moja kila mwaka na tani 300 za samaki, baada ya meli kubwa ya uvuvi wa bahari kuu kuanza kufanya kazi.

Akizungumza wakati akipokea meli hiyo inayoitwa Pacific Star inayomilikiwa na kampuni ya Al Bacora Group, katika Bandari ya Dar es Salaam, Waziri Ndaki alisema faida hiyo inatokana na serikali kuamua kufungua milango kwa wawekezeji wakubwa katika sekta ya uvuvi.

Alisema katika makubaliano hayo, kampuni hiyo inayomilikiwa na raia wa Hispania, itapewa leseni ya uvuvi na kupeperusha bendera ya Tanzania, itatoa mafunzo ya uvuvi kwa Watanzania watano na kujenga kiwanda cha kuchakata samaki nchini.

Waziri huyo alisema meli hiyo ya kisasa yenye uwezo wa kubeba tani 2,000 za samaki kwa mkupuo mmoja, itashughulika na uvuvi wa samaki wa aina ya Jodari katika Bahari Kuu ya Tanzania, Mauritias na Comoro.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuamua kufungua milango kwa wawekezaji wakubwa wa uvuvi kufanya kazi nchini kwetu, meli hii itatupatia faida kubwa za kiuchumi na hapa tumeanza kwani meli zingine zinakuja,' alisema.

Alisema katika mgawanyo wa mazao ya samaki, kampuni hiyo itatoa tani 200 za samaki aina ya Jodari na aina 100 zingine kila baada ya miezi minne, hivyo itapunguza pengo la ukosefu wa samaki. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame, alisema serikali zote mbili zina matumaini chanya na meli hiyo kwa sababu italeta mapinduzi mapya ya uvuvi baharini.

"Natarajia kila kitu kilichomo kwenye makubaliano kitatekelezwa kwa ukamilifu ili kila upande unufaike na rasilimali ya bahari, serikali zote mbili zinataka sekta ya uvuvi iwe uti wa mgogo wa uchumi wetu," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk.Christina Ishengoma, aliipongeza serikali kupitia Taasisi yake ya Bahari Kuu, kuipatia leseni kampuni hiyo kuvua samaki kwani itasaidia wananchi kupata chakula hicho kwa bei nafuu.



Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto (katikati), akijadiliana jambo na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma (kushoto), na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hoseah Kashimba, kabla ya makabidhiano ya kiwanda cha chai Mponde, kilichokuwa kimefungwa kwa takribani miaka 10, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMH**

# Serikali yakabidhi kiwanda cha chai Mponde kwa WCF, PSSSF

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

BAADA ya kushindwa kufanya kazi kwa takribani miaka 10 kutokana na sababu mbalimbali, hatimaye serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imekabidhi Kiwanda cha Chai Mponde kwa Kampuni ya Mponde Holding inayomilikiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya WCF na PSSSF iliyoomba kufanya uwekezaji na kukiendeleza.

Mifuko hiyo inamiliki hisa asilimia 84, kila mmoja ukiwa na asilimia 42 wakati asilimia zingine 16 zinamilikiwa na serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Makabidhiano ya kiwanda ikiwa ni pamoja na hati, mali na nyaraka mbalimbali yalifanyika jana jijini Dodoma kati ya Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto kwa niaba ya serikali na mwakilishi wa Mponde Holding Company ambaye pia ni Mkurugenzi wa Bodi ya Kampuni hiyo, Paul Kijazi. Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hoseah Kashimba na mwenzake wa WCF, Dk. John Mduma wa PSSSF, walikuwa miongoni mwa walioshuhudia makabidhiano hayo.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Mgonya alisema serikali imeona vyema mali na nyaraka zikakabidhiwa kwa uongozi wa Kampuni ili kuruhusu baadhi ya mambo muhimu yaliyohitaji nyaraka hizo kuendelea ili hatimaye shughuli za uzalishaji ziweze kuanza mara moja.

"Ofisi yangu inatoa shukrani za dhati kwa Bodi ya Mponde Holding pamoja na uongozi wa mifuko ya PSSSF na WCF kwa ushirikiano na jitihada kubwa mnazofanya katika kuhakikisha kiwanda cha Mponde kinarejea katika kuzalisha na hatimaye wananchi wapate ajira tena baada ya muda mrefu kupita.

"Ofisi yangu itaendelea kutoa ushirikiano stahiki kila itakapohitajika kwa lengo la kuhakikisha madhumuni yaliyokusudiwa katika kufufua kiwanda cha Mponde yanafikiwa," alisema.

Kiwanda hicho kilifungwa tangu mwaka 2013, baada ya mwekezaji katika Kiwanda cha Chai cha Mponde - Umoja wa Wakulima wa Chai Usambara (UTEGA) kukiuka masharti ya ubinafsishaji na serikali kujiridhisha pasipo shaka kwamba mwekezaji huyo hakuwa na mpango wala nia ya dhati ya kukiendeleza kiwanda hicho.

Kutokana na hali hiyo, serikali iliamua kukirejesha kiwanda kama Mkataba unavyoelekeza. Urejeshaji wa kiwanda hicho ulifanyika Januari, 2016.

Mbali na hati na nyaraka, Msajili wa Hazina pia amekabidhi magari matatu mali ya kiwanda hicho.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa kiwanda, mali na nyaraka hizo, Kijazi alishukuru serikali kwa uamuzi huo huku akiahidi kufanya kila linalowezekana kufikia malengo katika uwekezaji wao unaotarajiwa kuleta manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na ajira, kuendeleza zao la chai na pia kuchangia katika ukuaji wa pato la taifa.

# Mhasibu aliyeshtakiwa kuiba mil. 102/- aachiwa huru

**Na Kulwa Mzee**

ALIYEKUWA Mhasibu Kampuni ya SCI Tanzania Ltd, Monica Bwahama, ameachiwa huru baada ya Mahakama kuona upande wa Jamhuri umeshindwa kuthibitisha mashtaka 15 likiwamo la wizi wa Sh. milioni 102.

Mshtakiwa huyo aliachiwa huru jana na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Yusto Luboroga, baada ya kupitia ushahidi wa pande zote mbili.

Akisoma hukumu hiyo, alisema upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi 10 na mshtakiwa alijitetea mwenyewe.

Hakimu Luboroga alisema katika ushahidi uliotolewa na mashahidi hao, hakuna ushahidi ulioweza kumtia hatiani mshtakiwa, Mhasibu alipotoa ushahidi wake mahakamani alikana kuiba fedha hizo.

Mshtakiwa katika utetezi wake alidai kutoiba fedha hizo kwa kuwa yeye sio mweka saini na hakuwa na uwezo wa kuchukua fedha hizo, pia katika kipindi hicho hapakuwa na huduma ya fedha katika simu yaani simbanking.

Hakimu alisema mhasibu huyo pia alisema miamala yote iliyokuwa ikifanyika ilikuwa ikitumwa katika mfumo wa malipo na ilikuwa ikionekana na mahakama ilihitaji kuona nakala za miamala hiyo, lakini upande wa mashtaka ulishindwa kuwasilisha.

"Hakuna ushahidi uliooonesha kwamba fedha zilipotea bali imeonekana mshtakiwa alichanganya miamala badala ya kuingiza kwa X ameingiza kwa Y, hivyo mahakama inaona mshtakiwa hakuiba," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo mahakama imeona upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha mashtaka dhidi ya mshtakiwa na inamwachia huru.

Katika kesi hiyo mshtakiwa alikuwa akikabiliwa na mashtaka 15, 14 kati hayo yakiwa ya kughushi miamala ya fedha na moja la wizi wa kiasi hicho cha fedha.

Katika shtaka la wizi ilidaiwa kwamba kati ya Januari hadi Septemba mwaka 2013 katika Kampuni ya SCI Tanzania Ltd, Upanga, Monica aliiba Sh. milioni 102 mali ya Kampuni hiyo zilizofika kwake kutokana na nafasi yake ya kuajiriwa.

# Tanzania, Qatar kuimarisha ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri Mkuu wa Qatar, Sheikh Khalid bin Khalifa bin Abdulaziz Al Thani, kukubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta mbalimbali ikiwamo biashara ili kukuza uchumi.

Mazungumzo kati ya viongozi hao yalifanyika jana katika ofisi ya Al-Thani iliyoko Doha, Qatar.

"Ninamwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika vikao vyenye lengo la kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na Qatar na tumepata fursa ya kukutana na viongozi mbalimbali ikiwa ni mwendelezo wa ushirikiano kati ya nchi ya Tanzania na Qatar," alisema Waziri Mkuu jana baada ya mazungumzo hayo.

Alisema moja ya mambo waliyojadiliana ni uimarishwaji wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano ili kuongeza wigo wa maeneo mengi zaidi ya ushirikiano baina ya mataifa hayo, hivyo kutumia vyema fursa ya kuwa na ushirikiano mzuri wa kidiplomasia kwa miaka mingi.

Waziri Mkuu alisema kuwa kati ya mambo waliyoyawekea msisitizo ni pamoja na kuimarisha biashara kupitia Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Chemba ya Biashara ya Tanzania kupitia ushirikiano na wenzao wa Qatar na kwamba shughuli hizo zitaratibiwa na wizara husika ili kuhakikisha makubaliano hayo yanatekelezwa.

Alisema hivi karibuni kutakuwa na kikao cha pamoja cha wafanyabiashara wa Qatar ambao wameonesha nia ya kuja nchini Tanzania na kwamba serikali itawasimamia na kuwakutanisha na timu ya wafanyabiashara wa Tanzania kupitia TPSF ili wapate nafasi ya kujadiliana maeneo mengi ya uwekezaji. Majaliwa amesema mbali na kuimarisha uhusiano katika maeneo ya kibiashara na kisiasa pia viongozi hao wamekubaliana kubadilishana uzoefu kwenye sekta ya elimu ambapo wanafunzi wa Tanzania watapata fursa ya kwenda kusoma Qatar na wa Qatar kusoma nchini.

"Tunaendelea kuweka msisitizo wa ushirikiano kwenye maeneo ambayo yatatukuzia uchumi zaidi likiwemo eneo la utalii ambapo tunapata watalii wengi kutoka Qatar kupitia shirika la ndege la Qatar ambalo linaleta watalii wengi wanaopenda kuja kuona hifadhi ya Ngorongoro, Serengeti, Mlima Kilimanjaro pamoja na visiwa vya Zanzibar," alisema Majaliwa.

Maeneo mengine yaliyowekewa msisitizo katika mazungumzo hayo, kwa mujibu wa Majaliwa ni madini na kilimo ili kuhakikisha yanapata wawekezaji wengi.

"Pia Tanzania ni nchi ya pili yenye mifugo mingi Afrika, hivyo tumewaalika Wa-Qatar waje wawekeze kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo ili tupate soko la bidhaa hizo," aliongeza.



Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Kituo cha Iringa, Bryson Kamnde (kulia), akizungumza na waandishi wa habari kuhusu shughuli mbalimbali zinavyofanywa na mamlaka hiyo, walipotembelea katika ofisi za mamlaka hiyo, mkoani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wawili mbaroni madai uporaji fedha benki

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam linawashikilia watuhumiwa wawili wa ujambazi wanaodaiwa kujihusisha na vitendo vya kuwafuatilia na kuwapora fedha wateja wa benki.

Kamanda wa kanda hiyo, Jumanne Muliro, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia operesheni ya siku tano iliyoanza Machi 16, mwaka huu, mkoani humo inayoongozwa na taarifa fiche.

Alisema Jeshi la Polisi katika mahojiano na watu hao wamekiri kutumia pikipiki wanapowafuatilia watu benki na kwenye matukio mengine ya kihalifu wanayoyafanya.

"Watu hawa ambao ni Mussa Abdulrashid (28), mkazi wa Vikindu na Erick Mfuko (32) mkazi wa Kibamba, watuhumiwa kufanya vitendo vya kihalifu vya unyang'anyi wa kutumia silaha na wamekamatwa na bunduki mbili ambazo ni Browning yenye namba za usajili TZCAR113805 ikiwa na risasi tatu na Glock 15 yenye nambaTZCAR9611 ikiwa na risasi tatu kwenye magazine zake," alisema.

Vile vile, alisema silaha aina ya Glock 15 ina uwezo wa kuchukua risasi 15 na Browning risasi nane.

Pia wamekutwa na pikipiki yenye namba za usajili MC 123 DAL ambayo huitumia kwenye uhalifu huo.

Watuhumiwa hao wamekiri kuhusika kwenye matukio ya unyang'anyi kwa watu wanaotoka benki zikiwamo CRDB tawi la Kibada, Pugu Road na Temeke na NMB Banana na Airport.

Wamekiri kuwahi kumnyang'anya fedha Sh. milioni 30 mtumishi wa kampuni ya ASAS ambaye alikuwa ametoka kuzichukua benki.

Alisema mmoja wa watuhumiwa hao mwaka 2018 aliwahi kukamatwa na kupelekwa gerezani kwa unyang'anyi na baada ya miaka miwili kwa sababu za kisheria alitoka.

Kamanda Muliro alionya wanaojihusisha na vitendo hivyo mkoani humo kuwa Jeshi la Polisi likiwabaini hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.


JAMHURI YA MUUNGAMO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

OFISI YA MKUU WA MKOA IRINGA

Salamu za Pongezi

Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala Mkoa, Wakurugenzi na watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa mkoa na wananchi wote wa mkoa wa Iringa inayo furaha kuungana na Watanzania wote kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuadhimisha Mwaka mmoja madarakani.

KAZI IENDELEE...



H.E. Samia Suluhu Hassan

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Simu ; +255 262 702 715, Barua Pepe; ras@iringa.go.tz,Pawaga Road, Iringa

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari muhimu udhibiti wa kirusi kipya UVIKO-19

**WIZARA** ya Afya imetangaza kuwa inafuatilia uwapo wa aina mpya ya kirusi cha UVIKO-19 kilichothibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), na imeelekeza wataalamu wa afya kuangalia kama kimeshaingia nchini.

Hatua hizo zinachukuliwa kutokana na kwamba, kirusi hicho, kinajumuisha kirusi cha Delta na Omicron, ambacho kimejiunda na kuwa kirusi kipya cha Omicron BA.1, kimeshathibitishwa kuingia kwenye baadhi ya nchi. Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ndiye aliyetoa maelezo hayo kuwa, WHO inafanya utafiti wa kufahamu ukali wa kirusi hicho kipya, huku wizara yake nayo ikiendelea ufanya utafiti wa kuwapo kwa kirusi hicho nchini.

Pamoja na maelezo hayo, Waziri anawasihi Watanzania kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kujikinga na kirusi hicho, kwa kuwa watu wengi wakipata chanjo watasaidia kupunguza madhara ya ugonjwa huo utakapothibitika kuwapo nchini.

Sisi tunaungana na serikali katika harakati za kukabiliana na ugonjwa huo, ikiwamo kuchukua tahadhari zaidi ikiwamo kuhimiza watu kuchanja, kwani ni kweli kama anavyosema waziri kuwa hali ya uchanjaji bado ipo chini.

Kwani anasema, asilimia 66 ya wanaougua UVIKO-19 waliolazwa hospitalini hawajapata chanjo, hivyo tunaamini kuwa hali hiyo ni hatari kwa nchi, hivyo ingekuwa vyema kama wote tungeungana na serikali kukabili ugonjwa huo. Tunakumbusha kuwa Tanzania siyo kisiwa ambacho hakiwezi kufikika, bali ina mwingiliano wa watu kutoka maeneo mbalimbali nchini na hata nje ya nchi, hivyo suala la kujikinga na ujio wa kirusi hicho tunaona ni muhimu. Ikumbukwe kwamba Tanzania pia inapakana na nchi zaidi ya nane.

Kwa kuwa waziri anasema baadhi ya nchi zimeshatangaza kukumbwa na kirusi hicho, ni vyema na nchi yetu tukachukua tahadhari zote zinazoelekezwa na wizara husika kudhibiti mwingiliano wa watu kutoka mataifa mbalimbali.

Lakini tukumbushe msemo wa Kiswahili kwamba; 'ukimwona mwenzio ananyolewa, na wewe tia maji', hivyo Watanzania hatuna budi kuchukua hatua zote za kutuweka salama, ikiwamo kuchanja.

Njia nyingine ambayo tunadhani ni muhimu kuchukuliwa, ni kuangalia maeneo yote ambayo yanatumiwa na watu kuingia nchini, kuanzia mipakani, viwanja vya ndege, bandarini na hata vituo vya mabasi.

Tunadhani kwamba, kuna haja ya kuhakikisha watu wote wanaoingia nchini kupitia maeneo hayo wakapimwa ili kujiridhisha ikiwa ni njia mojawapo ya kudhibiti kirusi hicho kuingia Tanzania.

Kama tulivyoeleza kuwa Tanzania siyo kisiwa ambacho hakifikiki, ni wazi suala la Mtanzania kuchukua zote zinazoelekezwa na Wizara ya Afya kwa ajili ya usalama wa afya Watanzania, tunaona ni la msingi, si la kupuuza.

Hivyo, kwa kuwa serikali imekuwa ikisisitiza suala la chanjo na kuzingatia mwongozo wa Wizara ya Afya, basi tunashauri hatua hizo zichukuliwe na ikiwezekana serikali ifuatilie kwa karibu utekelezaji wake.

Tunajua kuwa suala la chanjo ni hiari, lakini kufuata mwongozo si hiari bali kinachotakiwa ni utekelezaji tu, kuanzia kunawa maji tiririka, kutumia vitakasa mikono, kuvaa barakoa na pia kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Iwapo jamii itazingatia mwongozo huo, huku kukiwa na udhibiti maeneo yote yanayotumiwa na wageni kuingia nchini, tunaamini kirusi hicho kipya kinaweza kudhibitiwa na kisipate nafasi.

Hivyo, tunashauri udhibiti huo pia uguse 'njia za panya' zinazotumiwa na baadhi ya watu wanaoingia nchini kinyemela ili kuhakikisha wote wanajulikana wasichangie kuingiza kirusi hicho kwa njia hizo bila wao kujulikana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Rais ameshaagiza, sasa kazi kwenu kutekeleza

**KILIO** cha watu wengi kimesikika, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kuagiza kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau kuhusu muundo wa tume huru ya uchaguzi.

Alitoa agizo hilo Ikulu, jijini Dar es Salaam juzi wakati akipokea taarifa ya kikosi kazi chenye wajumbe 25, kilichoongozwa na Mwenyekiti wake, Rwekaza Mukandala.

Rais alisema kuwa wajumbe hao wanatakiwa kuangalia maeneo kadhaa, ikiwamo maana na tume huru, iweje, pia kuangalia mifano ya waliokuwa na tume hizo kama wana migogoro au hawana, pia jinsi wanavyoziendesha.

Pia Rais Samia akaagiza kuboreshwa uhusiano baina ya vyama vya siasa na vyombo vya habari, ili kuwa na uhusiano wa karibu muda wote badala ya kuwaandika ifikapo kipindi cha uchaguzi pekee, lakini miaka minne inayobaki wanakuwa hawana uhusiano wa karibu kama ule wa mwaka wa mwisho wa uchaguzi unapokuja.

Kwanza, nimpongeza Rais Samia kwa kuruhusu kikosi kazi hicho kuanza kuratibu maoni kuhusu muundo wa tume huru.

Ni kitu ambacho kimekuja kwa muda mfupi mno na haikutarajiwa. Baadhi waliona ni kama hakitowezekana, au kitakuja baada ya muda mrefu baadaye.

Rais ameshatoa agizo na amemaliza kazi yake, sasa kilichobaki ni waliopewa jukumu hilo kutulia na kuanza kuratibu na kukusanya maoni taratibu ili yakirudi yawe si ya wanasiasa peke yake, bali ni ya wananchi wote, wenye faida kwa watu wote nchini na utamaduni wa Kitanzania.

Wafanye haraka haraka ili wamalize upesi kwa sababu fursa iliyosubiriwa kwa muda mrefu imepatikana, la hasha, ila watulie na warudishe maoni ambayo yakianza kufanya kazi yafanye kwa muda mrefu bila tena kuanza manung'uniko na mlalamiko, kuwa kuna mapungufu.

Kama alivyosema Rais, ni kwanza kabisa waanze kuangalia maana ya hiyo tume itakayoundwa, baadaye waangalie iweje, yaani muundo wake na waangalie mifano ya waliokuwa na tume hizo na jinsi wanavyoziendesha.

Kikosi kazi hicho sasa kinachotakiwa kuwa makini ni pale kwenye migogoro. Kama wana migogoro aliyobainisha Rais, wao watachotakiwa kuangalia hapo inasababishwa na nini, kwa sababu gani na hata kuainisha au kuangalia jinsi gani tume itakavyojiepusha na migogoro ambayo wenzetu wanayo.

Ni vizuri kwamba, wameanza na sisi tunaangalia wale ambao wameshapitia huko, hivyo tuna uwezekano wa kuwa na tume huru ya uchaguzi nzuri zaidi kwa sababu tutaona na kurekebisha mapungufu ambayo wenzetu wanayo.

Hii ndiyo fursa adhimu ambayo Rais ameitoa na haipaswi kufanyiwa masihara hata kidogo. Ni nadra sana kupatikana.

Kikosi kazi hicho sasa kinatakiwa kuangalie kwenye maeneo yote, na kisiegemee kwa wanasiasa pekee ambao ndiyo walioonekana au wanaoonekana kuhitaji zaidi tume hiyo kuliko kada zingine.

Ndiyo, wanasiasa wana upande wao kwenye hili, lakini iangaliwe pia, sehemu ya wapigakura ambao nao wanadamka asubuhi kwenda kushinda vituoni na kupiga kura kumchagua kiongozi anayempenda.

Kwenye hili pia mpigakura naye aangaliwe kwa jicho la pekee, ili kuwapa hamasa au hamu wananchi kwenda kupiga kura, kwani inaonekana kama kila miaka inavyozidi kusonga mbele wapigakura wanaanza kupungua.

Kikosi hicho kije na mapendekezo ambayo yanaweza kumfanya mpigakura hasa vijana ambao ndiyo kada inayodaiwa bado haijahamasika sana kupiga kura, kujiona wana umuhimu kwenda kumchagua kiongozi anayempenda, na si kuwaachia wazee tu.

TANGAZO

## Kesi mauaji ya mfanyabiashara madini yaahirishwa hadi Aprili 5

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mtwara, imeahirisha kesi ya tuhuma ya mauaji ya mfanyabiashara wa madini, Musa Hamis Hamisi (25), inayowakabili maofisa saba wa Jeshi la Polisi hadi Aprili 5, mwaka huu.

Kesi hiyo iliahirishwa jana baada ya upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Gideon Magesa, kuieleza mahakama kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Akiahirisha kesi hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Mtwara, Lugano Kasebele, alisema shauri hilo litarejea mahakamani hapo Aprili 5.

Watuhumiwa katika kesi hiyo ni Mrakibu wa Polisi ambaye alikuwa Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Mtwara, Gilbert Kalanje na Mrakibu Msaidizi wa Polisi, aliyekuwa mkuu wa Kituo cha Polisi Mtwara, Charles Onyango.

Wengine ni Mrakibu wa Polisi, aliyekuwa Mkuu wa Intelijensia Mkoa wa Mtwara, Nicholaus Kisinza, Mkaguzi wa Polisi, John Msuya, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Marco Mbuta, Mkaguzi wa Polisi, Shirazi Mkupa na Koplo Salum Mbalu.

Kwa pamoja, washtakiwa hao wanadaiwa kula njama na kisha kumuua mfanyabiashara wa madini Hamis Januari 5, mwaka huu, na kwenda kuutupa mwili wake katika kijiji cha Hiari, wilaya ya Mtwara.

Kwa mara ya kwanza, watuhumiwa hao walifikishwa mahakamani Januari 25, mwaka huu, baada ya kukamatwa na kuhojiwa katika vituo mbalimbali vya polisi kati ya Januari 22 na 24.

Musa anadaiwa kukumbana na kadhia hiyo ya mauaji wakati akidai zaidi ya Sh. milioni 33.7 zinazodaiwa kuchukuliwa na maofisa hao baada ya kumkamata Oktoba 20, mwaka jana, akiwa katika nyumba ya kulala wageni ya Sadina mkoani Mtwara.

# Bil. 58/- zilizoibwa ushirika zarejeshwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** ARUSHA

MALI zenye thamani ya Sh. bilioni 58 ambazo ziliuzwa kinyume cha utaratibu katika vyama vikubwa vya ushirika, zimerejeshwa kutokana na operesheni iliyofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC).

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na ambaye pia ni Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dk. Benson Ndiege, alisema hayo juzi katika kipindi cha dakika 45 kinachorushwa na luninga ya ITV kila siku ya Jumatatu.

Alisema mali hizo ziliuzwa katika miaka ya 1990 na 2000 ambapo kulikuwa na tatizo kubwa la wizi kwenye vyama vya ushirika hali iliyosababisha baadhi ya vyama kufa, hivyo kufanya utafiti na kutoa baadhi ya mapendekezo ikiwamo kuvihamisha vyama hivyo kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko wakati huo.

Dk. Ndiege alisema kuanzia 2010 hadi sasa, vyama vya ushirika vinafanya kazi vizuri kutokana na serikali kuweka msukumo wa kuviimarisha na kwamba kwa sasa hakuna mali za ushirika zinazouzwa kinyume cha utaratibu.

Alisema miaka ya nyuma kulikuwa na tatizo la vyama vya ushirika kukopa fedha kwenye benki na taasisi za kifedha na kushindwa kuzirejesha lakini hivi sasa umewekwa utaratibu kabla ya chama kuingia katika biashara yoyote, lazima kipate ridhaa kutoka kwa mrajis wa vyama vya ushirika.

Dk. Diege alisema TCDC imekuwa ikifanya tathimini mfano kama nyumba ya chama cha ushirika iliuzwa kinyemela ili kubaini makosa yalikuwa wapi na aliyehusika anawajibika kulipa kisheria na wale wanaostahili kunufaika na mali hiyo wanalipwa haki yao kwa mujibu wa sheria.

"Mfano kama kuna watu ambao waliibiwa kwenye SACCOS (Chama cha Kuweka na Kukopa) kwa kuweka pesa zao pale na viongozi wawili au watatu wakazitumia vibaya, ukweli ukibainika wanabanwa kisheria na wanazirejesha benki hatimaye wanufaika wanapewa haki zao," alisema.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha 2020 hadi 2021 TCDC kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Jeshi la Polisi, ilikusanya fedha nyingi ambazo ziliibwa kwenye SACCOS na vyama vya ushirika.

Kutokana na hali hiyo, amewaondoa hofu wananchi na kuwataka waendelee kujiunga na vyama vya ushirika na kuhakikisha wanawajibika kwa kushiriki kwenye vikao kwa kuwa wao ndio walinzi wakuu wa vyama vyao na serikali kwa upande wake itaendelea kuvisimamia.



Baadhi ya vijana wa Kanisa la Waadventista Wasabato la Mbezi Luis, mkoani Dar es Salaam, wakichangia damu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Matendo ya Huruma ya kanisa hilo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UDSM kuanza uzalishaji wa vifaranga

**Na Christina Mwakangale**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imewekeana saini na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) utekelezaji wa ujenzi na uendeshaji wa Kituo cha Taifa cha Rasilimali za Ukuzaji Viumbe Maji Bahari (NMRC), unaoanza kwa awamu ya kwanza kwa gharama ya Sh. Bil 1.59.

Kituo hicho kinatarajia kuzalisha samaki, kamba miti, kaa, majongoo bahari, chaza kwa tani zipatazo milioni moja hadi 2.5.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, aliyasema hayo jana katika mradi huo unaojengwa kwenye kampasi ya Kunduchi Shule ya Sayansi ya Viumbe vya kwenye maji na Teknolojia ya Uvuvi (SOAF) kupitia Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) na Benki ya Dunia (WB).

Alisema yapo mahitaji makubwa nchini ya vifaranga vya samaki pamoja na chakula chao na kwamba uzalishaji hauendani na mahitaji, akisema mwaka 2020/21 jumla ya vitotoleshi 33 vilitotolesha vifaranga milioni 22 huku hali halisi ya mahitaji ni milioni 115.

"Kituo hiki na vingine ni muhimu kwenye huduma za ukuzaji ugani, viumbe hai baharini kuunda na kutengeneza boti, kushona nyavu, kuzalisha vifaranga na vyakula vya samaki, kutengeneza vizimba na biashara ya samaki. Samaki huchangia takriban asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama," alisema Dk. Tamatamah.

Alisema wizara hiyo ina wajibu wa kuhamasisha, kuendeleza na kusimamia ukuzaji viumbe maji ili kuleta maendeleo ya kiuchumi ya mwananchi mmoja mmoja na taifa kupitia rasilimali maji inayotoa fursa kushiriki na kunufaika na uchumi wa buluu.

"Azma ya serikali ni kuona fursa za uchumi wa bluu zinatumika ipasavyo, kuleta ustawi kwa wananchi na kukuza uchumi. Mwaka 2020, sekta hiyo imetoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi wapatao 195,435 na wakuzaji viumbe maji 30,064 wakati watu zaidi ya milioni 4.5 wanajipatia kipato kutokana na shughuli mbalimbali katika minyororo ya thamani," alisema Dk. Tamatamah.

Aidha, Dk. Tamatamah alisema wafugaji wengi hasa wadogo wanalazimika kutumia mazalia ya kwenye mabwawa yao kama mbegu, hali ambayo haileti tija kutokana na vifaranga hivyo kukosa ubora.

"Kwenye chakula cha samaki, tulikuwa na viwanda 11 vilivyozalisha takribani tani 1,000 lakini mahitaji ni tani 27,000. Hapa pia, wafugaji hususani wale wadogo wanaishia kutegemea chakula cha asili cha kwenye mabwawa na pia kujitengenezea vyakula vyao na hivyo kuathiri tija," alisema Dk. Tamatamah.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. William Anangisye, alisema wakati nchi ikitarajia kukuza uchumi kupitia uchumi wa buluu, ni wakati wa kutatua changamoto za upatikanaji wa chakula cha viumbe hai, vifaranga ili kuwapo ufugaji wenye tija.

Mbunifu wa Majengo kutoka Wakala wa Majengo Tanazania (TBA), Paschal Kamata alisema mradi huo awamu ya kwanza utakamilika kwa miezi mitano ambao utakuwa na sehemu ya kutotolea na kukuzia vifaranga milioni 2.5 vya samaki wenye mapezi.

Pia, alisema mradi huo utakuwa na sehemu ya kuangulia mayai ya majongoo bahari na kukuzia vifaranga milioni moja pamoja na vifaranga vya kaa milioni moja.

# Mabaraza yaonywa uwekaji mazuio kuhusu uuzaji nyumba wadaiwa benki

**Na Munir Shemweta,**
SENGEREMA

SERIKALI imewataka wenyeviti wa mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya kujiepusha na tabia ya uwekaji mazuio yasiyo na tija dhidi ya uuzaji wa nyumba za wadaiwa wa benki.

Akizungumza wakati wa kuzindua Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Sengerema juzi jijini hapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema baadhi ya mazuio huwekwa na kisha shauri hupangiwa tarehe ya mbali bila sababu ya msingi.

''Jambo hili halikubaliki hata kidogo kwani linarudisha nyuma shughuli za kimaendeleo na kukuza uchumi wa nchi,'' alisema Dk. Mabula.

Alisema serikali inaendelea kutoa kipaumbele katika kuyawezesha Mabaraza ya Ardhi kufanya kazi vizuri na tayari imeanza kufanya maboresho ya muundo wa wizara utakaowezesha kila mkoa kuwa na msajili msaidizi wa mabaraza kwa ajili ya usimamizi wa karibu wa utendaji kazi wa vyombo hivyo.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali na katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, imefanya mabadiliko ya sheria ili kuwawezesha wenyeviti wa mabaraza kuwa na ajira za kudumu.

Aliwakumbusha watumishi wote wa mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya nchini kutimiza majukumu yao kwa weledi na kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyoko na ile itakayokuwa ikitolewa ili kuboresha utoaji huduma za utatuzi wa migogoro itokanayo na matumizi ya ardhi.

Pia Waziri Mabula aliwataka wenyeviti hao kuwafuata wananchi kwa kutembelea mabaraza mapya ili kusikiliza mashauri kwenye wilaya husika wakati wizara ikiendelea kukamilisha taratibu za ajira za wenyeviti wa mabaraza hayo.

Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Stella Tullo, alisema ofisi yake imejipanga na kuhakikisha migogoro ya ardhi inapofika kwenye mabaraza inasikilizwa kwa haki na kwa haraka na kusisitiza kuwa hawatopenda kuchelewesha mashauri bila sababu za msingi.

''Tunataka shauri linapofika kwenye baraza lianze kusikilizwa mapema baada ya taratibu za awali za kisheria kukamilika ili kukamilisha kwa wakati,'' aslisema.

Uzinduzi wa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Sengerema uliwakilisha pia uzinduzi wa mabaraza mengine mapya katika wilaya za Nachingwea, Ruangwa, Liwale, Kilwa, Serengeti, Kongwa, Kishapu na Mlele.



Wafanyakazi wa kiwanda cha bia cha Tanzania (TBL), tawi la Mwanza, wakisafisha mazingira kandokando ya Ziwa Victoria, eneo la Iloganzala, jijini Mwanza jana, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Maji Duniani. TBL ni mdau mkubwa katika utunzaji wa vyanzo vya maji na inaendelea kuwekeza katika miradi ya upatikanaji wa majisafi na salama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Operesheni za kushtukiza kuwa endelevu

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limetangaza kufanya operesheni za kushtukiza kutafuta bidhaa hafifu za chakula na vipodozi zinazopatikana katika masoko mbalimbali.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Meneja wa Shirika hilo Kanda ya Magharibi, Rodney Alanga, wakati akizungumza kuhusu operesheni ya ukaguzi wa bidhaa za chakula na vipodozi

Alisema kwenye operesheni hiyo watashirikiana na vyombo vingine vya serikali kama vile Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), uongozi wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri.

TBS, ilisema itafanya operesheni hizo za kushtukiza katika maeneo ya masoko mijini, vijijini, mipakani, bandarini na kuwabaini wakiukaji na kuchukua hatua za kisheria ili kulinda afya ya watanzania, biashara na mazingira.

Hivi karibuni, alisema TBS Kanda ya Magharibi ilikamata bidhaa za chakula na vipodozi zenye uzito wa tani 32.2 zikiwa na thamani ya Sh. 97,706, 200 katika operesheni maalumu iliyofanywa katika halmashauri 11 za mikoa ya Katavi, Rukwa na Kigoma.

Alisema ilifanyika kwenye maghala, maduka makubwa ya jumla na rejareja, mipakani na bandarini.

Alanga alisema lengo la operesheni hiyo ilikuwa kuondoa bidhaa hafifu zinazopatikana katika masoko ya mikoa ya kanda ya magharibi ili kuwalinda walaji wa bidhaa hizo na madhara yanayoweza kujitokeza.

Alisema kwa sasa inatarajia kufanya uteketezaji wa bidhaa hizo baada ya taratibu zote za kisheria kufuatwa.

"TBS imechukua hatua za awali kwa kuzuia bidhaa zote zilizoonekana kuwa na makosa ambazo utekelezaji na ufuatiliaji wake utaendelea ndani ya siku 14 kwa mujibu wa notisi ya kuzuia bidhaa," alisema Alanga.

Kwa mujibu wa Alanga, oparesheni hiyo ilibaini makosa yanayofanywa na wafanyabiashara kwa kuuza bidhaa za chakula na vipodozi ambazo zimekwisha muda wa matumizi, zisizosajiliwa na TBS na uuzwaji wa vipodozi vilivyopigwa marufuku kutumika.

Alisema katika operesheni hiyo changamoto kubwa iliyobainika ni wafanyabiashara wengi kupitisha bidhaa kwa njia za panya, kutokagua bidhaa katika maduka yao kuhakiki muda wa mwisho wa matumizi, kutotunza kumbukumbu za manunuzi na mauzo.

# Walalamikia mikopo kiduchu halmashauri

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

KIKUNDI cha watu wenye ulemavu kinachojishughulisha na ufugaji wa nguruwe Kitangili Manispaa ya Shinyanga, kimeomba kiwango halisi cha fedha zinazoombwa katika halmashauri badala ya kupewa pungufu.

Mtunza Hazina wa kikundi hicho, Janet Limbe, alisema hayo juzi wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii katika mahojiano maalum namna fedha za mikopo ya halmashauri zilivyomsaidia kusomesha watoto wake hadi chuo kikuu.

Alisema anaishukuru serikali kwa utoaji wa mikopo hiyo ya asilimia 10 ambayo ni asilimia nne kwa vijana, nne kwa wanawake na mbili kwa watu wenye ulemavu, hivyo kutoa rai kwa serikali iwe inatoa fedha hizo kama zinavyoombwa na vikundi kwa kuwa zinakuwa zimeombwa kulingana na bajeti na malengo.

"Sisi katika kikundi chetu cha watu wenye ulemavu hapa Kitangili ambao tunafuga nguruwe, tuliomba mkopo wa Sh. milioni tano lakini tukapewa Sh. milioni tatu, fedha ambazo tulishindwa kukamilisha mipango yetu," alisema Limbe.

Alisema mpaka sasa kikundi chao kina nguruwe 28 wenye watoto saba na walianza ufugaji huo mwaka 2018, baada ya kupata mkopo wa Sh. milioni mbili kutoka Halmashauri na kununua nguruwe wawili ambao walizaliana na mwaka jana ndipo wakapata mkopo mwingine Sh, milioni tatu na kuendelea kuboresha ufugaji huo.

Limbe alisema nguruwe wanapokuwa wengi huwa wanauza na kisha kugawana fedha ambazo wanazitumia kukidhi mahitaji yao ya nyumbani ikiwamo kusomesha watoto kwa kuwatimizia mahitaji yao ya shule kwa wale wa sekondari na mwingine kumlipia ada ambaye anasoma ngazi ya stashahada katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

Mmoja wa watoto wa mwanamke huyo mwenye ulemavu wa macho, Ndiganya Michael, ambaye anasoma chuo kikuu na sasa yupo Shinyanga kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo, alisema anaishukuru serikali kwa utoaji wa mikopo hiyo ambayo itatimiza ndoto zake na kuwasaidia wazazi wake na wadogo zake.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Shinyanga, John Tesha, alisema kwa mwaka jana kuanzia Julai hadi Desemba, walitoa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu yenye jumla ya Sh. milioni 175.

Hivi karibuni, Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, akiwa mkoani Shinyanga, aliagiza wakurugenzi katika mikopo kwa makundi maalum, wawe wanatoa fedha nyingi kwa vikundi vichache, kuliko kutoa fedha kidogo kwa vikundi vingi ambazo hazikidhi mahitaji yao.

HABARI KITAIFA

# Mabula aonya wanaodanganya kulipwa fidia

**Na Munir Shemweta,**
SENGEREMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewaonya wananchi wanaojenga au kupanda mazao kwenye maeneo yanayopangwa kutwaliwa na serikali kwa shughuli mbalimbali zikiwamo za uwekezaji maarufu kama 'tegesha' baada ya kutangazwa tarehe ya ukomo ya kufanya maendelezo.

Alitoa onyo hilo wilayani Sengerema mkoani Mwanza wakati wa uzinduzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Sengerema.

Alisema, kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wananchi kununua maeneo yaliyopangwa kutwaliwa na serikali kwa ajili ya shughuli mbalimbali na kuanza kufanya maendelezo ya kujenga ama kupanda mazao ili kupata fidia wakati wa zoezi la uthamini, huku maeneo hayo yakiwa yametangazwa tarehe ya ukomo ya kufanya maendelezo.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, serikali haitavumilia tabia hiyo kwa kuwa jambo hilo linaiingizia hasara serikali na kusisitiza kuwa, wananchi watakaobainika kufanya vitendo vya tegesha basi watachukuliwa hatua kali ikiwamo kufikishwa kwenye vyombo vya sharia.

"Mtu anapanda mualovela mlimani na inaonekana wenyewe umechomekwa, nisisitize kuwa, kama kuna kitu kilichoongezeka baada ya kuchukuliwa picha ya anga na kutangazwa kwa tarehe ya ukomo ya maendelezo basi hakitalipwa na serikali italipa kile kinachoonekana kwenye picha ya anga," alisema.

Dk. Mabula alitolea mfano kwa eneo la Mlima Nyanzaga wilayani Sengerema kuwa kuna baadhi ya wananchi wamenunua eneo la mlima na kuanza kusafirisha migomba nyakati za usiku ili kutegesha kwa lengo la kupata fidia baada ya kusikia serikali inataka kulitwaa eneo hilo.

Alisema, hali hiyo haiwezi kuvumiliwa na serikali italipa fedha kwa yale maeneo yaliyoonekana katika picha za anga ambazo Wizara ya Ardhi ilizichukua mapema kwa lengo la kuondoa mgongano wakati wa kulipa fidia.

Kuhusu uzinduzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Sengerema, Waziri Mabula alisema uzinduzi wa baraza hilo umelenga kusogeza huduma kwa wananchi wa wilaya hiyo ya Sengerema ambao awali walikuwa wakiifuata wilayani Geita.

Aliwataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi kwenye wilaya ambazo Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya hayajaanza kutoa huduma, kutoa kipaumbele kwa shughuli za mabaraza kwa kutenga maeneo ya ofisi kuwezesha mabaraza kuanza kutoa huduma ili kuwaondolea wananchi usumbufu wa kwenda kupata huduma katika wilaya nyingine.

## Maelfu kunufaika na mradi wa maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI 12,488 wa kata nne za Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga wanatarajia kunufaika na mradi wa maji wa Ziwa Victoria unaotekelezwa na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa thamani ya Sh. bilioni 2.035.

Wananchi hao ni kutoka katika vijiji vya Mwakuzuka Kata ya Mwanase, Kabondo Kata ya Kashishi, Izuga kata ya Jana pamoja na kijiji cha Mwashigina kata ya Mwakata na kila kijiji kitajengewa tenki la maji lenye ujazo wa lita 90 na kuuziwa maji kwa bei nafuu.

Aidha, kati ya vijiji hivyo kijiji cha Kabondo na Mwakuzuka wanaendelea kunufaika na majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria baada ya kujengewa matangi mawaili ya maji kwa thamani ya Sh. milioni 821.

Kaimu Meneja wa RUWASA wilayani Kahama, Paschal Mnyeti, aliyabainisha hayo jana mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa maji wa kijiji cha Mwakuzuka na Kabondo.


Alisema utekelezaji wa miradi hiyo umeanza tangu Machi, mwaka 2018 na unatarajia kukamilika ndani ya miezi 12.

Alisema, mradi huo utakapokamilika unatarajia kuwanufaisha zaidi ya wananchi 12,488 katika vijiji hivyo na kwamba kwa sasa wanaendelea kujenga matangi maji yenye ujazo wa lita 90,000.

Diwani wa Mwanase, Samson Masanja, aliomba miradi hiyo kukamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa sababu wananchi wanatumia maji ya visima walivyochimba kwa kuchangia na mifugo yao hali ambayo inaweza kusababisha kutokea kwa magonjwa ya mlipuko ikiwamo kuhara damu.

DC Kiswaga aliwataka wasimamizi wa mradi hiyo kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa wananchi ili kuwaondolea wananchi shida ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma ya majisafi na salama.

Alisema wananchi wengi ndoa zao zimeingia shakani kutokana na wanawake wengi kuamka alfajiri kwa ajili ya kusaka maji na kuacha wanaume wamelala jambo ambalo linaweza kuondoa uaminifu.




Waziri wa Nishati, January Makamba (wanne kushoto), akizindua nembo mpya ya Total Energy, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## LAAC yabaini stendi Njombe inavyokosesha mapato

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Hesabu za Serikali (LAAC), Grace Tendega, amewaagiza viongozi mkoani Njombe kukubaliana kutotumia stendi ya mabasi ya mjini ambayo inahatarisha usalama wa abiria kutokana na kuwa kwenye hifadhi ya barabara katikati ya mji.

Agizo hilo limetolewa baada ya kutembelea miradi ya mabasi pamoja na soko mjini hapa na kuwa licha ya changamoto hiyo pia uwapo wa stendi hiyo unaikosesha mapato halmashauri.

"Halmashauri mhakikishe katika maeneo yenye kasoro za ujenzi zikiwamo nyufa kwenye barabara za magari makubwa stendi kuu na sakafu katika jengo la mama ntilie zinarekebishwa kufikia mwezi Juni," alisema Grace.

Awali akiwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi wa stendi na soko, Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Mji, Shigela Ganja, alisema imefanikisha utekelezaji wa ujenzi wa stendi na soko kupitia Programu ya Uimarishaji na Uboreshaji Miji (ULGSP) na kufanikiwa kupata Sh. bilioni 20 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Ganja alisema, licha ya mradi wa stendi na soko kubabadili mandhari ya mji na kuwezesha mazingira bora ya kutolea huduma, bado changamoto ya utekelezaji wa mradi umeshindwa kuzaa matunda yaliyokusudiwa kutokana na kuwapo na stendi katikati ya mji na kusababisha abiria wengi kuishia mjini.

Kamati hiyo imekagua na kutembelea katika stendi ya mabasi Njombe na soko kuu kujiridhisha na utekelezaji wa matumizi ya fedha zilizotengwa kwenye miradi hiyo.

Changamoto hiyo ya ufanisi wa stendi uliwaibua wajumbe wa kamati hiyo akiwamo Twaha Mpembenwe, aliyesema idadi ya mabasi ni ndogo na wananchi wanaotumia stendi hiyo na vibanda kushindwa kukodishwa.

Katika hatua nyingine Katibu wa CCM Mkoa wa Njombe, Ally Mwinyi, alisema chama hakipo tayari kuona mwananchi akionewa na halmashauri ikipoteza mapato kwa kuwa serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa stendi mpya, na kuelekeza matumizi ya stendi yaendelee kama ilivyokuwa wakati ikiwa inaanza kwa kufuta kituo cha msaada cha sasa kilichoko stendi ya zamani.

# Kemikali 3 marufuku uzalishaji vipodozi

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limepiga marufuku matumizi ya kemikali za aina tatu kwenye uzalishaji wa vipodozi kwa sababu ya kuhusishwa na kuathiri mifumo ya uzazi pamoja na kuhusishwa na saratani. Marufuku hiyo ilitangazwa na Msimamizi wa Dawati la Usajili wa Majengo ya Bidhaa za Vyakula na Vipodozi wa TBS, Moses Mbambe, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na usimamizi wa bidhaa hizo unavyofanyika.

Mbambe alitaja kemikali zilizopigwa marufuku kwenye uzalishaji wa vipodozi kuwa ni Pyrithione Zinc (anti-dandruf agent) na Butylphenyl methylpropional (lilial) ambazo zinahusishwa na kuathiri mifumo ya uzazi, huku kemikali aina ya Sodium Hydroxymethylglycinate ikihusishwa na saratani.

"Kwa hiyo kuanzia Machi 1, mwaka huu tumeanza kuzuia. Zipo bidhaa nyingi za Perfume (manukato) zina kemikali hiyo zikifika tunazizuia usajili wake," alisema Mbambe.

Kwa upande wa vipodozi, Mbambe alisema wanaangalia vitu ambavyo haviruhusiwi kutumika katika kuzalisha vipodozi. Aidha, alisema kuna vitu vingine haviruhusiwi kutumika kwenye uzalishaji wa vipodozi na vile vinavyoruhusiwa kwa kiwango fulani wanaangalia kama wazalishaji wamekidhi kutumia kiwango kile ambacho wazalishaji wanahitaji.

"Pale ambapo vipodozi vitakidhi basi vitasajiliwa na TBS na vitaruhusiwa kuingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya binadamu lengo likiwa ni kuwalinda watumiaji wa bidhaa ili wasitumie bidhaa ambazo kesho na kesho kutwa zitakuja kuathiri afya zao," alisema.

Kuhusu usajili wa bidhaa za vyakula na vipodozi kutoka nje ya nchi, Mbambe alitoa mfano kwamba wamekuwa wakikataza au kusajili vipodozi ambavyo vinaingizwa nchini vikiwa na viambata vya sumu.

"Vipodozi hivi haviruhusiwi kutumika katika soko la hapa nchini. Vipodozi hivi tunakutana navyo sana, zipo kemikali ambazo haziruhusiwi kutumika katika vipodozi, lakini utakuta zinatumika," alisema.

Mbambe alisema usajili wa majengo pamoja na bidhaa za vyakula na vipodozi ni takwa la kisheria kwa mujibu wa sheria ya viwango Sura Na: 130, ambapo kwa utaratibu wa ndani wa shirika, wameelekeza kwamba bidhaa zote za chakula na vipodozi ambazo zinaingizwa nchini lazima zitafanyiwa usajili.

Kwa upande wa zile bidhaa vyakula na vipodozi ambazo zinazalishwa ndani ya nchi, alisema zinafanyiwa ithibati ya ubora, na kwamba usajili huo unafanyika lengo likiwa ni kuhakikisha ubora na usalama wa hizo bidhaa.

"Bidhaa zote zinazoingizwa nchini mwagizaji anapaswa kujisajili kama mwagizaji wa bidhaa za chakula na vipodozi, kusajili ghala ambalo atakuwa anatumia kwa shughuli za uhifadhi bidhaa za chakula na vipodozi, lakini vile vile kusajili bidhaa za chakula," alisema.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia (kulia), akimsikiliza mkunga wa mkoani Shinyanga, Flora Kajumla, baada ya kumkabidhi tuzo ya Mwanamke wa Shoka katika sekta ya afya kwenye tuzo za 'Kitchen Party Gala 2022', zilizoandaliwa na EFM, jijini Dar es Salaam juzi. Taasisi hiyo kupitia mradi wake wa M-Mama inawasaidia wanawake wajawazito mkoani humo kutumia simu zao za mkononi kuunganishwa na huduma ya dharura ili kuokoa maisha yao na ya mtoto kwa kupatiwa usafiri pindi wanapopatwa na uchungu pingamizi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima korosho wadaiwa mamilioni

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAKULIMA wa Chama cha Ushirika wa Mazao na Masoko Mkundi Amani (AMCOS) wilayani Masasi mkoani Mtwara wanadaiwa madeni ya fedha za mkopo wa pembejeo za kilimo walizokopeshwa msimu uliopita wa zao la korosho wa mwaka 2021/2022 zaidi ya Sh. milioni 97 na taasisi mbalimbali za kifedha.

Fedha hizo ni kutoka katika taasisi mbalimbali za kifedha ikiwamo benki, ambapo taasisi hizo zilichukua dhamana ya kuwakopesha wakulima hao kabla ya msimu huo kuanza lengo likiwa ni kuwasaidia wakulima kupata pembejeo za kilimo kwa wakati.

Hayo yamebainishwa jana na katibu wa chama hicho, Fadhili Hassani, alipokuwa akisoma taarifa ya utendaji kazi ya chama hicho kwa msimu wa zao la korosho wa mwaka, 2021/2022 katika mkutano mkuu wa 14.

Fadhili alisema chama hicho kwa sasa kimekuwa na mzigo mkubwa wa madeni katika taasisi za kifedha yanayotokana na baadhi ya wakulima ambao walikopeshwa pembejeo za kilimo na taasisi hizo katika msimu wa ununuzi wa zao la korosho wa mwaka,2021/2022 ambapo hadi sasa fedha hizo hazijalipwa.

Alisema miongoni mwa taasisi hizo ambazo zinawadai baadhi ya wakulima wa chama hicho ni Benki ya CRDB ambayo inadai Sh. milioni 70, YETU BENKI inadai zaidi ya Sh. milioni 13 pamoja na Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima Masasi-Mtwara(MAMCU) kinachodai Sh. milioni 14.5.

"Wakulima kwa sasa hawezi kukopesheka tena kwa sababu walio wengi bado wanadaiwa mikopo ya pembejeo ya msimu uliopita wa mwaka 2021/2022 , fedha ambazo wakulima wetu wanadaiwa ni jumla ya Sh. milioni 97.3, na hii inatoa picha mbaya kwa chama chetu cha ushirika,"alisema Hassani.

Fadhili alisema baadhi ya wakulima wamekuwa wagumu kulipa madeni yao ya pembejeo za kilimo ambazo walikopa kwa hiari yao, hivyo kusababisha chama kuwa katika nafasi mbaya ya kutokopesheka na taasisi hizo hivyo kukosa fursa ya kupata misaada mbalimbali ikiwamo pembejeo za kilimo.

Aliwataka wakulima wote ambao bado wanadaiwa fedha za mikopo kuanza kulipa madeni yao haraka ili katika kuelekea msimu ujao chama kisipoteza fursa ya kukopesheka kwa mara nyingine kwa wakulima ambao hawana madeni.

Ofisa Ushirika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Shaibu Mvita, alisema mzigo huo wa madeni kwa chama hicho ni mkubwa na wanachama ambao wanadaiwa wanapaswa kulipa mikopo yao ili kukifanya chama kiepuke kuwa na mzigo wa madeni.

Mvita alivitaka vyama vya ushirika ambavyo wanachama wake wanadaiwa mikopo ya pembejeo za kilimo kulipa madeni yao ili kuwa na fursa ya kukopa tena msimu ujao wa 2022/2023.

## Vodacom yaeleza inavyorahisisha malipo ya maji

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA kuadhimisha Wiki ya Maji Duniani, kampuni ya mtandao wa simu ya Vodacom Tanzania Plc imeeleza jinsi inavyosaidiana na serikali kurahisisha upatikanaji wa maji nchini kwa njia ya kidigitali.

Imetoa maelezo hayo katika kilele cha Wiki ya Maji ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Maji Duniani, chini ya kauli mbiu 'Maji Chini ya Ardhi, Hazina isiyoonekana kwa Maendeleo Endelevu'.

Mkurugenzi wa M-Pesa, Vodacom Tanzania, Epimack Mbeteni, alisema, inaungana na serikali katika kuhakikisha kuwa malipo yanafanyika kidigitali.

"Kama sote tunavyofahamu, serikali yetu imeweka dhumuni la kuhakikisha Tanzania inakuwa ya kidijitali hasa kwenye malipo ya Ankara mbalimbali zikiwamo za serikali," alisema Epimack.

Alisema Vodacom inaamini kupitia huduma ya M-Pesa, mwananchi atafanya malipo yatakayowezesha upatikanaji wa maji kwa huduma endelevu ikiwamo kulipia huduma mbalimbali za serikali

"M-Pesa inawezesha watumiaji zaidi ya milioni 1.6 nchini kulipa ankara zao za maji kidijitali kwenda kwa taasisi 23 za maji katika mikoa yote nchini na kufikisha malipo ya Sh. bilioni 36 kwa mwaka," alisema.

Alisema huduma hiyo inaokoa muda kwa mtumiaji na kuzipa taasisi husika nafasi ya kufanya shughuli zingine. "Tunataka kuona wateja wetu na Watanzania kwa ujumla wakiokoa muda, hakuna sababu ya wao kupanga foleni kulipia ankara za maji ilhali anaweza kulipia kupitia simu yake ya mkononi, M-Pesa tupo hapa kuboresha maisha ya Watanzania wote," aliongeza Mbeteni.

## Ajitosa uhamasishaji chanjo ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

MWEZESHAJI wa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana nchini, Aman Matungullu, amejitosa katika uhamasishaji wa chanjo ya UVIKO-19 kwa vijana anaowapa elimu ili kuwanusuru dhidi ya ugonjwa huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matungullu alisema, amekuwa akisafiri katika mikoa mbalimbali nchini kutoa mafunzo ya ujasiriamali, lakini ndani ya mafunzo hayo anahamasisha chanjo. "Nimeona kampuni yangu iitwayo Matungullu's Production Ltd ya jijini Dar es Salaam, inayojihusisha na mafunzo ya ujasiriamali, itumike pia kuhamasisha vijana kuhusua suala la chanjo ya corona," alisema.

Alisema yeye kama kijana ameona kuna haja ya kufanya sehemu yake kwenye suala la kujikinga na ugonjwa huu, kwa kuwakumbushia vijana wake kuchukua hatua za chanjo.

""Jukwaa langu la kuhamasisha vijana wenzangu ni kuchanja ni kupitia mafunzo ya ujasiriamali ambayo nimekuwa nikiyatoa kwao katika maeneo mbalimbali nchini," alisema.



Ukurasa 12

**MAPENDEKEZO YA KIKOSI KAZI**

## Wadau wadai sheria zifumuliwe, katiba mpya isisubiri 2025



Ukurasa 13

Kinamama wasomeshwa Mbozi wakaelewa, sasa waongoza mitaa



Ukurasa 14

## Rais, profesa na babu aliyeachiwa huru kutoka kifungo cha hadi 2032


**siasa**

JUMATANO MACHI 23, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


# Je, Ujamaa upo au umetoweka?

**Na Peter Orwa**

HISTORIA ya dunia kwa muda mrefu, iligawanyika kisiasa katika kambi kuu mbili, mkondo wa kushoto ambako ndiko penye Ujamaa na kulia ndio mfumo huria au ubepari.

Katika ngazi ya juu penye mamlaka zilizoshika dunia, mkondo wa kulia uliongozwa na Umoja wa Kujihami wa NATO, hali kadhalika Mashariki, ni iliyokuwa Warsaw Pact, wadau wa Ulaya Mashariki.

Ingawa kumekuwapo na mijadala ya kudadisi tafsiri kamili, kambi na itikadi; kinachojulikana kambi ya Magharibi ilijikita kwenye mfumo huria katika uchumi, hata siasa na itikadi, ambao kwa kiasi kikubwa wananufaika na kodi, vingine vikibaki katika mikono binafsi.

Hapo serikali inabaki kuwa mratibu mkuu wa mifumo huria na kushika maeneo machache ambayo ama yanagusa au yana manufaa ya moja kwa moja kwa umma, mathalan penye elimu na afya.

Hali kadhalika, inaangukia miradi yenye maslahi na tafsiri ya moja kwa moja kwenye maisha ya umma, mathalan mifumo ya usafiri kama reli, barabara na anga. Lakini kwa kiasi kikubwa serikali inanufaika na kupata pato la kujiendesha kupitia kodi.

Kinyume chake, mfumo hodhi wenye mlengo wa kushoto au wa kijamaa umekuwa na sura ya serikali kujihusisha moja kwa moja na maisha ya umma, kuanzia umiliki wa rasilimali, uendeshaji wake, hata itikadi zao za kijamii.


Sura nyingine inayotoa tofauti, kati ya makundi hayo mawili ni kwamba, wakati mfumo huria au wa kibepari uliojulikana wakati huo, umeegemea kutoza kodi kidogo, lakini katika kila kitu ambayo Wamarekani wana msemo :hakuna cha bure Marekani."

Mfumo hodhi kijamii- wa kijamaa, wenyewe unatoza kodi kubwa, huku serikali ikiwajibika moja kwa moja kuhudumia watu wake, hasa huduma muhimu kama elimu, afya na mahitaji muhimu ya kijamii.

Hata hivyo, wakati ulipofika kukaanguka kambi ya Mashariki hasa ngome ya Warsaw Pact mwanzoni mwa miaka ya 1990, kuna mchango katika kudidimiza dhana ya Ujamaa na itikadi yake duniani.

Kukashuhudiwa hata baadhi ya nchi, kama Checkslovakia kuanguka kisiasa na kugawanyika sehemu mbili.

Katika siasa hii itakumbukwa hata kabla ya hapo, Tanzania ikawa miongoni mwao, nchi nyingi zilizopata uhuru zilijielekeza katika mkondo huo, zikiamini kuna sehemu kubwa ya wananchi wake wanahitaji kukombolewa kiutawala, kisiasa na kiuchumi.



Mwalimu Julius Nyerere. **PICHA: MTANDAO**

**UKWELI ULIKOFIKIA**

Maana ya msamiati huo, ujamaa na hoja yake ni swali lenye utata nchini na hata kimataifa, hasa baada ya kuzama ngome hiyo kuu ya Warsaw Pact.

Kuna wakati lilijitokeza katika kada ya wanasheria nchini walipohojiwa na iliyokuwa Tume ya Jaji Kisanga, kupata maoni yao, chini ya aliyekuwa kiongozi wakati huo, Bob Makani, wakapendekeza kufutwa kwa kipengele cha Ujamaa kwenye katiba.

Hata hivyo, kabla ya kupokea hoja yao, meza kuu ya wana - tume hiyo, wakawahoji "kwani Ujamaa una maana gani?" Ni swali waliloshindwa kujibu wajumbe wote, kwenye kikao kilichofanyika kwenye ukumbi, jijini Dar es Salaam.

Hata swali aliporejeshewa mzee wao Bob Makani, naye alikwama kutoa ufafanuzi hata hoja hiyo ikafa na wakusanya maoni wakisema hawatochukua hoja ambayo wakati wenyewe hawakujua maana yake.

Hiyo ikiangaliwa kwa kina, hakuna tafsiri ya pamoja inayotolewa kuhusu dhana ujamaa. Hata hivyo, kinachokubalika kwa wakati mmoja, ni kwamba "jamii inapoishi katika matazamio ya kundi linaloshirikiana na kujaliana, kwa manufaa ya pamoja, baadhi kufika hatua hata rasilimali zao nyingi wanazimiliki kwa pamoja."

Ndani ya mtazamo huo, utekelezaji wa dhana hiyo ya kisiasa na kiitikadi unatajwa kuwa na sura kuu tatu, ambayo walikuwa nayo wanazuoni wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na waumini wake wakubwa; wote sasa marehemu; maprofesa kama Haroub Othman, Mwesiga Baregu, Wamba dia Wamba, na Sethy Chachage, waliuhubiri sana.

Profesa Othman, aliuhubiri Ujamaa wa Kiafrika, Tanzania ikiwa na msingi wa tafsiri kutoka kwa Mwalimu Nyerere, kwamba 'watu wanakaa pamoja, wanafanya kazi, kwa faida ya wote.'

**INAENDELEA UK. 14**

MAPENDEKEZO YA KIKOSI KAZI

# Wadau wadai sheria zifumuliwe, katiba mpya isisubiri mwaka 2025



Mkurugenzi wa LHRC, Anna Henga, akizungumzia mapendekezo ya kituo hicho kwa kikosi kazi. Kulia ni Ofisa Programu Wanawake na Watoto wa kituo hicho, Getrude Dyabene. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

KIKOSI kazi kilichoundwa na Msajili wa Vyama vya Siasa kuratibu mapendekezo ya wadau wa vyama vya siasa nchini, na imeyakabidhi kwa Rais Samia Suluhu huku ikitaka mchakato wa katiba mpya uanze baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Sababu ya kutaka mchakato wa katiba mpya uanze baada ya uchaguzi huo, inaelezwa na Mwenyekiti wa Kikosi Kazi hicho, Prof. Rwekaza Mukandala, kuwa, muda huo ni mwafaka hautaathiri uchaguzi mkuu ujao, ikipendekeza kufanyiwa maboresho kwenye sheria na kanuni za uchaguzi nchini.

**KUTOKA LHRC**

Nipashe imezungumza na wadau wa demokrasia ya vyama vya siasa, ikiwamo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambacho Mkurugenzi Mtendaji wake Anna Henga anasema wamefanya mchakato kwa maana ya kuja na maoni kadhaa ikiwamo kuruhusiwa matokeo ya kiti ya urais kupingwa mahakamani ikiwa kuna malalamiko ya msingi, kuwapo mgombea binafsi na mfumo wa mshindi awe na kuanzia asilimia 51.

"Tunachukulia kama ilivyoamuliwa na Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu katika kesi ya Jebra Kambole dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Na. 018/2018," anasema Henga.

Mkurugenzi huyo anasema, kutopinga matokeo ya urais ni kinyume na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981.

> Katika mkutano huo wa Baraza la Vyama vya Siasa sisi wadau ndiyo tulioshauri msajili aunde Kikosi Kazi hicho baada ya suala la katiba mpya, hivyo tulitakiwa kwanza tuyaone mapendekezo hayo.

Kuhusu mgombea binafsi, anasema ni hatua inayoendana na uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu ya Watu, katika kesi iliyofunguliwa na Mchungaji Mtikila.

"Mahakama hiyo iliruhusu mgombea binafsi, nasi tunatambua kuwa kuwapo utaratibu huo, kutasaidia kupunguza urasimu wa vyama vya siasa ambavyo hutumia sifa za uanachama dhidi ya wagombea, inapotokea kutoelewana kati ya pande mbili," anasema.

Anaendelea: "Jeshi la Polisi lisiingilie shughuli za vyama vya siasa wakati, kabla na baada ya kampeni kinyume na sheria. Kuwe na watumishi wa tume ya uchaguzi, wakurugenzi wa halmashauri wasisimamie uchaguzi."

Anataja mapendekezo mengine kuwapo mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa kufanyika kwa usawa, pia nafasi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iwe ya kutangazwa hadharani kwa vigezo vitakavyoainishwa na kamati maalum ya kuajiri.

"LHRC, pia inapendekeza mkurugenzi wa uchaguzi, mwenyekiti wa tume ya uchaguzi na makamishna wapatikane kwa kuomba kazi ambazo zinatangazwa hadharani.

"Uteuzi wa wajumbe wa tume ya uchaguzi uzingatie uwakilishi wa vyama vikubwa vya siasa, asasi za kiraia, taasisi za kidini na wanataaluma. Kigezo cha kupita bila kupingwa kiondolewe....," anasema, akitaja pia haja ya kuwapo mfumo wa kielektroniki kupiga kura.

Mkurugenzi Mtendaji huyo anasema kituo chake kinapendekeza umuhimu wa takwa la kisheria kwa vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia na watu wenye ulemavu wakati wa mchakato wa uteuzi.

**MTAZAMO WA CUF**

Magdalena, Naibu Katibu Mkuu (Bara wa chama CUF, anasema anashangaa kuona suala la upatikanaji katiba mpya linasogezwa mbele, badala ya kuharakisha ipatikane kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Anafafanua kikosi kazi kilichoundwa na Msajili wa Vyama vya Siasa, kilitakiwa kwanza kupeleka mapendekezo kwenye Baraza la Vyama vya Siasa kabla ya kufikishwa kwa Rais.

"Katika mkutano huo wa Baraza la Vyama vya Siasa sisi wadau ndiyo tulioshauri msajili aunde Kikosi Kazi hicho baada ya suala la katiba mpya, hivyo tulitakiwa kwanza tuyaone mapendekezo hayo," anasisitiza.

Mwanasiasa huyo anasema katika mkutano wa msajili na baraza hilo Desemba mwaka jana jijini Dodoma, kuliibuka hoja kama ya katiba mpya na kusababisha kuundwa kwa kikosi kazi hicho.

"Kilikuwa na jukumu la kupitia hoja zilizojitokeza katika mkutano huo na kuandaa mapendekezo kwa ajili ya kuwasilisha kwenye Baraza la Vyama vya Siasa ambalo lingeyapitia na kuyawasilisha serikalini," anasema.

"Hali hiyo ndiyo ilisababisha sisi kutangaza kususia uchaguzi wowote hadi pale katiba mpya itakapopatikana na huo ndiyo msimamo wetu na tulitegemea kikosi kazi kije na jibu la kukata kiu ya wadau," analalamika.

Naibu Katibu Mkuu huyo anasema, CUF itaitisha vikao kujadili mapendekezo hayo hasa suala la katiba mpya, kwa madai kwamba ikiwekwa pembeni hadi baada ya uchaguzi mkuu ujao, si matakwa ya wadau. Hata hivyo hakufafanua kikao kipi.

**MAONI YA JUKATA**

Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba, Bob Wangwe, anasema kwa mtazamo wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), anapinga mapendekezo hayo, akitamka:

"Katiba mpya inasaidia kupata tume huru uchaguzi, hivyo hatuoni sababu za msingi za kuahirisha mchakato huo wakati katiba inayopendekezwa ipo."

Wangwe anasema, Watanzania wanataka katiba mpya na kwamba hilo ndilo hitaji la wengi ambalo lilipaswa kufanyiwa kazi haraka kwa kumalizia mchakato ulioshia njiani baada ya Bunge Maalum la Katiba.

Mkurugenzi huyo anasema, JUKATA itaendelea kutoa wito wa kuwapo kwa katiba mpya, kwa madai kwamba siyo hitaji ya kikundi cha watu wachache bali ni matakwa ya Watanzania.

"Suala la kuwapo kwa katiba mpya halitakiwi kucheleweshwa, hivyo nitoe wito kwamba, tuendelee kupigania katiba mpya na huo ndiyo msimamo wa Jukwaa la Katiba Tanzania," anasema.

**KUVUTA SUBIRA**

Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia Kurasini Dar es Salaam, Godwin Gonde, anasema kilichobaki sasa kwa hatia iliyofikiwa ni Watanzania kuwa na subira, kwa madai kwamba kila upande umepewa ahadi.

"Wanaotaka katiba mpya wameahidiwa kuwa mchakato utafanyika baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 na wale wanaotaka uchaguzi upite nao wameahidia, hivyo kilichobaki ni subira tu,"anasema Gonde.

Anafafanua, mchakato wa katiba mpya una gharama kubwa ikiwamo fedha, si jambo la kuharakisha na kwamba inawezekana kikosi kazi hicho kiliangalia yote na kutoa mapendekezo.

"Hata kama hoja itakuwa ni kwamba, tayari katiba inayopendekezwa ipo, ni lazima tutambue kuwa wakati mwingine baadhi ya mapendekezo yanaweza kuwa yamepitwa na wakati au inahitajika kuongeza mengine," anasema.

Anasema mwaka 2014 hadi sasa ni miaka mingine imepita na kuna mabadiliko makubwa ambayo yanaweza kusababisha hata katiba inayopendekezwa ikafanyiwa mabadiliko, na kwamba hatua hiyo inahitaji muda wa kutosha.

"Kwa hiyo ushauri wangu ni kwamba, muda ambao umependekezwa na kikosi kazi hicho, ni bora ukaheshimiwa kwa kuacha mihemko ya kisiasa ili wakati ukifika, mchakato wa katiba mpya ufanyike," anasema.

KAZI INAVYOENDELEA

# Kinamama wasomeshwa Mbozi wakaelewa, sasa waongoza mitaa

**Na Beatrice Philemon, aliyekuwa MBOZI**

RAIS Samia Suluhu Hassan, tangu aingie madarakani amekuwa akidumisha usemi unaobeba utashi wa kinamama, jinsia yao inapopewa usukani kuendesha umma, mara zote wanufaika ni jamii nzima kwani 'umama' hujitokeza dhahiri.

Kwa kutathmini yaliyojitokeza kwa mwaka mmoja uliopita na kusherehekewa Jumamosi iliyopita, pana kidokezo cha ushahidi wahitaji wote wa elimu ya juu wamehakikishiwa mkopo tena katika mazingira nafuu zaidi.

Simulizi hiyo inajiashiria, pia kwa uongozi wa kinamama ngazi ya chini kupitia ushahidi wilayani Mbozi, mkoa wa Songwe katika kata za Hasamba na Itaka, kura za udiwani na baadhi ya nyadhifa vijijini, matunda yako wazi wapigakura wako 'meno nje'.

Ziara ya Nipashe ya wilayani Mbozi hivi karibuni imebaini namna mama madiwani na wenzao wajumbe wa halmashauri ya vijijini wanawahakikisha 'kazi iendelee.'



Jukwaa la Wanawake Mbozi wakijadiliana masuala ya uongozi katika mradi wa usimamizi wa uwajibikaji jamii katika masuala ya ugani. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON**

## DIWANI AFUNGUKA

Costina Kibona, ni mama mwenye watoto watatu kutoka kata ya Hasamba. Ni kati ya wanakijiji walionufaika na mradi uitwao "Kuimarisha Uwajibikaji Jamii na Usimamizi katika Sekta za Afya (VVU/Elimu ya Uzazi) na Kilimo (Usalama wa Chakula) Kusini mwa Afrika."

Ni mradi wa miaka mitano unaotekelezwa na Shirika la MIICO na Action Aid Tanzania katika vijiji vitano; Iyula, Itaka, Zelezeta, Hasamba na Idiwili kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC).

Baada ya kupata mafunzo ya uongozi, haki za mwanamke, watoto, jinsia, kilimo na ikolojia, mwaka katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Costina alijitosa kuwania udiwani na akafanikiwa kwa kishindo.

Mama huyo ambaye sasa ni Makamu Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, anajigamba kuleta maendeleo kwa kata, pia wanawake wote.

Anajivuna kuwafungua fikra za wapigakura wake, umuhimu wa kushiriki mikutano ya hadhara, kwa sababu ni haki yao kujua kinachoendelea katika jamii yao.

Costina anasema, ana mchango kufanikisha kujengwa zahanati katia Kata ya Hasamba, pia kuwezesha huduma za kinamama kujifungua, tofauti na ilivyokuwa nyuma.

Anasema wahitaji walitembeea umbali kilomita nane hadi 10 kwenda kujifungua kwenye Hospitali ya Wilaya Mbozi, wengi walisafiri kwa bodaboda kwenda na kurudi Sh. 4,000 na wasiokuwa nazo walijifungua majumbani.

"Niliamua kusaidia upatikanaji wa huduma hii kwa sababu, najua machungu ya mama kujifungua yalivyo, athari ya usafiri na kipato cha wananchi kilivyo kidogo katika kata yangu," anasema.

Katika elimu, anadokeza baada ya kuona kuna mrundikano mkubwa wa wanafunzi katika shule zilizoko katika eneo lake, anasema Diwani Costina baada ya kuingia madarakani, akaanza kufanya kazi na wananchi kujenga madarasa 17 ya shule za msingi, pia sekondari.

Hapo anaorodhesha ujenzi wa madarasa sita katika Shule ya Sekondari Ndugu, matatu shule ya Namile, matano shuleni Muungano na matatu Shule ya Msingi Ilyika, huku kukiwapo miradi mingine katika hatua tofauti. Hapo, anadokeza akaiomba Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kusaidia hatua za kumalizia ujenzi, nguvu zao zilipogota.

"Nashukuru serikali kuu imeniletea shilingi milioni 40 ambazo zimesaidia kukarabati vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Sekondari Ndugu kwa kushirikiana na nguvu za wananchi," anafafanua.

"Wakati wa Mbio za Mwenge, viongozi walikuja kukagua na wakaridhika na vimezinduliwa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Josephine Mwambashe," anasema.

Pia, anataja kuwapo miradi aina hiyo inayoendelezwa katika ujenzi wa majengo ya shule za msingi, ikiwamo mabati mapya zaidi ya 300 kutoka vyanzio mbaliombali vya kiserikali na fedha taslimu Sh. milioni 12.5.

## KUHAMASISHA KINAMAMA

Pia anasema kupitia elimu aliyoipata kutoka Shirika la Action-Aid Tanzania na MIICO, amehamasisha vikundi vya wanawake na vijana kupitia mikutano ya hadhara ya kata, vijiji na vitongoji wajiunge kwenye vikundi vya ujasiriamali, ili waweze kupata mikopo kutoka kwenye halmashauri .

"Nashukuru hadi sasa vikundi viwili vya kinamama kutoka kitongoji cha Hazelu A na Kamshikeni, vimepata mkopo," anataja baadhi, pia vingine vikijumuisha vijana.



Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani Mbozi, Costina Kibona.

## MJUMBE HALMASHAURI KIJIJI

Esther Ngao, ni mzazi mwenye watoto wanne, anasema katika katika uchaguzi uliopita wa Serikali za Mitaa Mwaka 2019, alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

Anasema wako 25 waliopenya kutoka orodha ya wagombea 86, kati yao wako kimamama 10 wanaoongoza vitongoji: Itaka, Masewe, Lunyego na Shiha.

Nini amefanya kazini? Anaifafanulia Nipashe kwamba: "Toka nichaguliwe nimesaidia wanawake katika kijiji cha Itaka kuboreshewa soko ili kufanya biashara katika mazingira mazuri."

Pia anasema amefikisha hoja ya viwanja vya makazi na hadi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi serikali ya kijiji imeshatoa viwanja 100 vya makazi kwa vijana na taratibu zake za ramani zimeshafanyiwa kazi.

"Nashukuru Shirika la MIICO na ActionAid Tanzania kutupatia elimu hii, kwa sababu kinamama hivi sasa wanajua haki zao, wanaweza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

"Wanaweza kusimama na kuhoji kuhusu fedha zilizotengwa na serikali kwa ajili ya maendeleo ya kijiji, kitongoji au kata kama zimetumika vizuri au la," anasema.

Mjumbe huyo wa kijiji anaendelea: "Nina ujasiri wa kusimama na kuongea hoja, naweza kuuliza bajeti zilizoko katika kijiji chetu kama zinatekelezwa au hazitekelezwi tofauti na miaka ya nyuma, nilikuwa naogopa kusimama na kuuliza."

Anaeleza wana ujasiri wa kielimu, kujiamini, kujua haki na kugombea nafasi za uongozi kwenye nafasi za ubalozi au uenyekiti unaojitokeza kwenye maeneo yao, kijijini au zaidi ya hapo.

> Tunajivunia kuona nafasi ya mwanamke kuweza kusema changamoto zao kwa viongozi bila woga tofauti na miaka ya nyuma kabla ya kupata mafunzo na kujua haki zao.

## WALIOWAWEZESHA

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la MIICO, Catherine Mulaga, anaorodhesha matunda yao kwamba katika ngazi ya uongozi walipatikana madiwani wawili kupitia Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, kata za Hasamba na Itaka kukiwapo wajumbe 12 wa halmashauri za kijiji.

"Tunajivunia kuona nafasi ya mwanamke kuweza kusema changamoto zao kwa viongozi bila woga tofauti na miaka ya nyuma kabla ya kupata mafunzo na kujua haki zao.

"Miaka ya nyuma kinamama wengi walikuwa hawawezi kusimama mbele ya viongozi na kutoa changamoto zao zinazowakabili," anaeleza Catherine ambaye pia ni mwanamama.

"Hivi sasa chochote kinachopangwa kuhusiana na maendeleo ya kijiji lazima wanawake washirikishwe na ongezeko limeongezeka kutoka asilimia 10 hadi 70 ya mahudhurio," anasema.

Anafafanua kuwa, kabla ya mafunzo kinamama wengi hawakujua haki zao, hawakudhuria mikutano na waliohudhuria wachache sana, hawakuongea, lakini sasa hali imebadilika wanashiriki na kutoa hoja, pia wanagombea nafasi za uongozi zinazojitokeza.

"Sasa hivi serikali imeweza kusogeza huduma za mikopo vijijini tofauti na zamani, kinamama walijua kuwa shughuli za kilimo hazikopesheki, lakini sasa hivi baada ya mafunzo wanafanya shughuli za mikono wanaweza kutumia fedha hizo," anasema.

## JUKWAA LA VIONGOZI

### MJUE ALBERTO FUJIMORI

# Rais, profesa na babu aliyeachiwa huru kutoka hukumu hadi 2032

**Na Christina Mwakangale**

- Mwaka 2017 aliachiwa, akarejeshwa gerezani
- Amestaafu uamishoni na akanaswa huko huko
- Bintiye kawania urais 'nikipita, namtoa baba'



Alberto Fujimori. **PICHA: MTANDAO**

WIKI iliyopita kulishuhudiwa kuachiwa kutoka gerezani kwa aliyekuwa Rais wa taifa la Peru na msomi profesa wa uhandisi, Alberto Fujimori Inomoto, aliachiwa kutoka gerezani akiwa babu wa miaka 83.

Hiyo ni historia nyingine, akitoka katika maisha ya kutaabika na kudhalilika, ilhali kati ya mwaka 1990 hadi 2000, alikuwa mkuu wa nchi kwa cheo cha urais.

Kiongozi huyo wiki hii aliachiwa kutoka kifungoni baada ya mahakama ya juu ya kikatiba kutoa agizo hilo, huku hisia zikiwa tofauti miongoni mwa jamii, rais wa sasa Pedro Castillo, anayetaka mahakama ya kimataifa iingilie suala hilo.

Uamuzi huo unawakumbusha Waperu msamaha wa kibinadamu uliotolewa kwa Fujimori katika Mkesha wa Krismasi mwaka 2017, kutoka kwa Rais wa wakati huo, Pablo Kuczynski.

Wakati alipopewa msamaha hapo awali, aliyekuwa rais miaka ya 2027, Kuczynski, akasema Fujimori amestahili msamaha kutokana na hali yake kiafya ikiwamo matatizo ya moyo.

Fujimori, alihukumiwa kifungo gerezani kutokana na shtaka la kukiuka haki za binadamu na rushwa, pia iwapo angetumikia kifungo chote angekuwa huru mwaka 2032; sasa mahakama hiyo imemwondolea adhabu hiyo.

Fujimori, siku ya Alhamisi wiki iliyopita ilikuwa ya kipekee kwake baada ya kuachiwa huru, katika hukumu iliyoendana na majaji walipopiga kura kutoa uamuzi huo, ingawa haikuwa wazi lini Fujimori angeondoka gerezani.

Rais Fujimori, ambaye kitaaluma anajulikana kuwa mbobevu katika hisabati, umaarufu wake ulianza mwaka 1990 alipowania urais na kumshinda katika uchaguzi mtangulizi wake, Mario Vargas Losa, ambaye kitaaluma ni mwanahabari.

> Lengo la Rais Fujimori wakati huo, lilikuwa kugombea urais wa Peru tena mwaka 2006, badala yake aliangukia kwenye kesi na hata kuhukumiwa gerezani.

Alipoingia tu katika mamlaka nchiji Peru, kukashuhudiwa kupigwa hatua kwenye uchumi wa nchi, akiegemea zaidi sera huria kwa kuzibinafsisha kampuni na viwanda.

Hata hivyo, urais wake uliangushwa muda muda mfupi baada ya kuingia katika zama za awamu ya tatu, baadaye mwaka 2000, ikaonekana video yake ikionyesha Ofisa Usalama Mkuu wake, Vladimiro Montesinos, akiwahonga wanasheria.

Wakati huo Rais Fujimori akiwa mapumzikoni nchini Japan ambako ndiko kwenye asili ya wazazi wake, akatuma barua pepe kwa faksi kuelezea kujiuzulu kwake baada ya tukio hilo.

Miaka mitano baadaye, aliwashangaza wafuasi na maadui wake kisiasa, aliposafiri kwa ndege hadi nchi jirani ya Chile ambako alikamatwa na kurejeshwa nchini Peru.

Lengo la Rais Fujimori wakati huo, lilikuwa kugombea urais wa Peru tena mwaka 2006, lakini badala yake aliangukia kwenye kesi na hata kuhukumiwa gerezani. Binti yake, Keiko Fujimori, aliwania urais mwaka jana huku akitoa wito baba yake kuachiwa huru na akasema iwapo angeshinda, angemtoa baba yake kifungoni, hata hivyo alishindwa na Pedro Castillo.

Kwenye mashtaka yaliyomsibu, Fujimori ametuhumiwa na mashtaka yanayotokana na jukumu lake katika programu ya serikali ya miaka ya 1990, ambayo wanawake wengi wenye asili kutoka jamii maskini, walisema walilazimishwa kuzaa watoto.

Tuhuma nyinginezo zikahusu mauaji ya wakulima sita, yaliyodaiwa kufanywa na wanajeshi, katika zama za utawala wake.

Fujimori ni mzaliwa wa Julai 28, 1938 mjini Lima, Peru amehudumu urais tangu Julai 28, mwaka 1990 hadi Novemba 19, mwaka 2000.

Asili yake ni Japan, akitoka katika familia ya mhamiaji nchini Peru, ambako amesoma na kupata elimu shahada ya kwanza katika Chuo cha Agrarian, mwaka 1961, kisha akapiga hatua zaidi na kung'ara ngazi ya uprofesa.

**ALIVYOINGIA KATIKA SIASA**

Amejiunga na siasa kwa mara ya kwanza mwaka 1989, akiwa mkuu wa chama kipya wakati huo kilichoitwa Cambio 90 (kwa maana ya 'Mabadiliko 90').

Ushindi wake katika urais ulikuwa wa kushangaza, mwaka 1990 na mwaka 1992. Kashfa ya mwaka 2000 baada ya uchaguzi mwaka huo, ikimhusisha ofisa wake, imesababisha kukimbia uhamishoni nchini Japan.

Mwaka 2005 Fujimori, ameenda nchini Chile, ambako alikamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi kwa ombi la taifa la Peru.

Miaka miwili baadaye akiwa bado gerezani, aligombea kiti katika bunge la Japan bila ya mafanikio. Baada ya mvutano wa muda mrefu kisheria, akahamishiwa nchini Peru mwaka 2007.

Miaka miwili baadaye, akafikishwa mahakamani alikokabiliwa na mashtaka manne tofauti, hata akaangukia hatia ya kutumia vibaya mamlaka yake, hali kadhalika dai la rushwa.

Baada ya hapo, Fujimori, ambaye ni baba wa watoto watano, akahukumumiwa kifungo cha miaka 44 na miezi mitano.

## Je, Ujamaa bado upo au umetoweka?

**INATOKA UK. 11**

Pia, msomi Haroub Othman, anataja aina ya pili ni Ukomunisti; huo ni ujamaa unajitokeza katika sura iliyopiga hatua zaidi katika mfumo wa pamoja.

Hapo inagusa miliki za mali na uchumi, itikadi ukisimamiwa kwa kina mifumo ya kisheria, ambayo ilipatikana zaidi ndani ya ngome ya Warsaw Pact katika Ulaya Mashariki na maraiki zao kama vile China, Cuba.

Sura ya tatu, Prof. Othman, anaeleza katika namna serikali katika mfumo huria, inajiegemeza zaidi na kuwajibika moja moja klwa m;pja na maslahi ya umma, mtazamo unaofafanuliwa na mwanazuoni Dk. Alfred Lokuji akitumia mifano:

"Serikali inadumu kuwa sehemu ya jamii na mara zote haijabaki nyuma katika kuwakamua na shida zao dhidi ya matesi kutoka nguvu ya soko huria."

Mfano hai, uko katika vyama vyama vya siasa vya Labour nchini Uingereza an Democrat, ambao sehemu kubwa ya sera zao ni katika setrikali kuwajibikia mopja kwa moja shoda za umam inabopibi. Kwa lugha nyingine, zinajisogeza kwenye mlengo wa kushoto kitikadi.

Itakumbukwa, hata chanzo cha chama cha Labour cha Uingereza, haitofautianii sana na mzizi wa saiasd za Afrika, vyama vyau siasa vilipoanza, kwani kundi la wafanyakazsi walioteswa naa mapinduzi wa viwanda, walitaka utetezi.

Hapo ndipo, kukajitokeza jamii iitayo 'Fabian Society' ambao walikikuwa waumini waa maoni na fikra za wafanyakazi, wakawaunga mkono hata kuzaliwa chama hicho, pia sheria za kazi zinazotawala dunian kote sasa.

Vivyo watetezi hjao wa wati wa chini kutaka wajaliww na serikali ndi kilichoko kwa chama cha Democrat, haa kukishuhiwa na Rais Barack akitumia hoja ya kuhuishwa bima ya afya kuwanusuru watu wa chini.

Nchini Tanzania, ikirejewa tiokadi ya waassisi wea nyendo za chama TANU kuanzia TAA, kama fami,ia ya Sykes, hawakutofautiana sana an Fabian Societu kabal uaya kuimbna ubia wa kina Mwalimu Nyerere, kisha akapata ubia wa wafanyakazi, ambako Rashid Kawawa, aliku3a Katibnu Mkuu w3a chjama chao.

Kuna ushuhuda wa sera mbalimbali nchini baada ya uhuri, ndani ya mfumo huria uliorejeshwa mwaka 1992, baada ya kufutwa mwaka 1964, marais wa karibuni Hayati John Magufuli na Samia Suluhu Hassan, wakiwa na mfano wa maboresho.

Mathalan ni katika elimu bure jadi kufikia kidato cha nne, huku elimu ya juu kufungulikwa fursa zaidia za mikopo rafiki kwa elimu ya juu.

Vyote hivyo ni viashria tofauti vya Ujamaa katika ulingo tofauti, serikali ikijiegemeza kuelekea mlengo wa kushoto, kama anavyotafsiri Dk. Lokuji: "Serikali ijabaki kiuwa sehyemu nja kuachia ielemewe na nguvu ya soko (huria)..."



## TACAIDS yataka usimamizi kufundisha VVU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa vijana wenye umri wa miaka 14 hadi 24, Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), imewataka Maofisa Elimu na Wakaguzi wa Elimu kusimamia walimu kufundisha masuala ya VVU na Ukimwi, Afya ya Uzazi, Stadi za Maisha na Uviko-19.

Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya elimu ya VVU na Ukimwi, afya ya uzazi na stadi za maisha, UVIKO-19 kwa walimu wa shule za msingi na sekondari wa Wilaya ya Chamwino mkoani hapa.

Mafunzo hayo ni moja ya afua zinazotekelezwa katika mradi wa 'Timiza Malengo' ambao unalenga kupunguza maambukizi ya VVU kwa wasichana balehe na wanawake vijana wenye umri wa miaka 10 hadi 24 walio shule na nje na unatekelezwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Kifua Kikuu, Malaria na VVU na Ukimwi Global Fund.

Dk. Maboko alisema mafunzo hayo yanalenga kuwawezesha walimu kutumia miongozo ya kufundisha elimu hizo kwa shule za msingi na sekondari.

Alisema hadi sasa halmashauri 14 zimefikiwa na walimu wa shule za msingi 1,961 na sekondari 3,923 wamepewa mafunzo.

"Sasa maambukizi mapya nchini yanatokea kama watu 68,000 kwa mwaka, yaani watu 186 kwa siku, bahati mbaya sana ya vijana wanaopata maambukizi mapya ya VVU ni wa kike. Ukipiga mahesabu kati ya vijana 100 walioambukizwa VVU hapa nchini, 80 ni wa kike," alisema.

Alisema takwimu hizo ziliwafanya kuumiza kichwa wafanye nini kuhusiana na vijana katika maambukizi mapya na ndipo walipoamua kuja na mradi huo.

Dk. Maboko alisema akiangalia takwimu za umri wa kuanza vitendo vya ngono zinamtisha na baadhi zinaonyesha kuwa wanaanza vitendo hivyo wakiwa na miaka nane.

"Kwasababu watoto wanawasikiliza sana walimu na hivyo tukaona wawafundishe elimu ya VVU na Ukimwi," alisema.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Gladness Kirei, alisema watoto wamekuwa na wa sasa wapo katika wakati mgumu kwa kuona mambo mengi kwenye televisheni.

Naye Mratibu wa Mafunzo hayo kutoka Mamlaka ya Elimu Nchini (TET), Beatus Mapunda, alisema mamlaka hiyo ilipopata taarifa kutoka kwa TACAIDS waliandaa mwongozo wa mafunzo kwa kuwashirikisha wadau ikiwamo Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

# Waomba Rais Samia kuunda tume kufuatilia mgogoro wa wawekezaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameombwa kuunda tume ya kufuatilia mgogoro uliodumu kwa muda mrefu wa wawekezaji na wananchi katika kitalu namba 10 cha Kagoma Complex kilichoko Muleba mkoani Kagera ambacho kipo chini ya Shirika la Ranchi la Taifa (NARCO).

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, mmiliki wa kitalu hicho, Hashimu Luholera, alisema mgogoro huo ulianza tangu 2008 hadi sasa bado haujapatiwa ufumbuzi na umezidi kuwa mkubwa hali inayosababisha uharibifu wa mali ndani ya kitalu.

"Hali ya uwekezaji ni mbaya katika vitalu tunahatarisha usalama wetu na mazingira ya wawekezaji, tunaomba Rais uunde tume ambayo itafuatilia mgogoro huo, tunahitaji kuona unakwisha ili wawekezaji waweze kutimiza majukumu yao kirahisi bila bugudha yoyote na kujiinua kiuchumi," alisema Luhorela.

Alisema pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji kufika katika eneo la vitalu zaidi ya mara tatu kufuatilia mgogoro huo na kukabidhiwa nyaraka zote zinazohusu tatizo hilo, lakini hakuna utatuzi uliofanyika.

"Wawekezaji tuomba suala hili serikali iingilie kati na kulimaliza kabisa ili kuepuka kuleta athari ya maisha ya raia wanaoishi katika maeneo hayo," alisema Luhorela.

Alisema wamiliki wa vitalu, wanatambua juhudi zinazofanywa na Rais Samia na wanaomba mgogoro huo, utatuliwe ili watekeleze majukumu yao na kujiinua kiuchumi.

Alisema wamiliki wa vitalu vya NARCO wanatambua juhudi zinazofanywa na serikali hasa katika kuwalinda wawekezaji wa ndani na nje ili kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya nchi.



Meneja wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama Kanda ya Kati, Dk. Katura Mathias (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, akiwataka kuhamasisha Watanzania kujitokeza kuchangia damu. Wengine ni maofisa uhamasishaji wa damu salama, Edith Senga (kushoto) na Bernadino Medaa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# NGO zatakiwa kushirikiana na serikali kuondoa sheria kandamizi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Kutetea Haki za Ardhi nchini (LANDESA) limeyaasa mashirika yasiyo ya kiserikali kushirikiana pamoja na serikali kuhakikisha wanaondoa sheria kandamizi zinazochangia kumrudisha nyuma mwanamke.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Dk. Monica Mhoja, aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa 66 wa kimataifa wa kuangalia kamisheni ya hali wanawake hususani katika masuala ya umiliki wa ardhi (CSW 66), ulifanyika kwa njia ya mtandao na kuongozwa na Balozi wa Tanzania nchini Marekani, Prof. Gaston Kennedy.

Mkutano huo umeratibiwa na Shirika lisilo la kiserikali la Landesa, Oxfam kwa kushirikiana na serikali na ulishirikisha mashirika 25.

"Serikali imeziweka sheria hizi vizuri tu, lakini kuna baadhi ya maeneo ipo mifumo dume ambayo inawakandamiza wanawake ambayo tunapaswa kuikemea," alisema Dk. Mhoja.

Alisema mashirika yakiungana kupiga vita unyanyasaji, yatafanikisha kuondoa sheria kandamizi kwa wanawake hususani wa maeneo ya vijijini.

Alisema LANDESA wanaendelea na kampeni ya 'Linda Ardhi ya Mwanamke' ili kuondoa vikwazo vilivyoko katika umiliki wa ardhi ikiwamo mfumo dume. Alisisitiza kuwa LANDESA itaendelea kushirikiana na serikali ili kuhakikisha jamii za kitanzania zinatambua umuhimu wa kumiliki na kutumia ardhi kwa kufuata sheria na taratibu, ikiwamo kutoa elimu kwa jamii ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya tabia ya nchi.

Naye Mkurugenzi wa Jukwaa la vyanzo asilia Tanzania (TNRF), Zacharia Faustine, alisema katika suala la ardhi kuna vikwazo mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabia ya nchi na kwa kutumia teknolojia wanajaribu kuzitatua kero hizo.

Alisema kwa kushirikiana na serikali na taasisi nyingine zisizo za kiserikali, watahakikisha wanaondoa kero zinazowakandamiza wanawake na jamii kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Tike Mwambipile, alisema ili kuhakikisha wanawake wanajua haki yao ya kumiliki ardhi, wamejikita kumtazama mwanamke, kufuatilia sera, kutoa elimu na kuhakikisha wanawake wanapata haki zao za msingi katika jamii.



# TMDA yasaidia dawa vituo vya huduma

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imekabidhi dawa zenye thamani ya shilingi 20,859,400 katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe na Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kutumika katika vituo vya afya na zahanati za mikoa hiyo.

Dawa zilizokabidhiwa ni ambazo zilikamatwa zikiuzwa kinyume cha sheria katika maduka ya dawa muhimu nchini (DLDM).

Akikabidhi dawa hizo kwa niaba ya Meneja wa Kanda, Mkaguzi Msaidizi, Seleman Mayala, alisema kuwa dawa hizo zilikamatwa kwenye ukaguzi ambao ulifanyika mikoa ya Mbeya na Songwe katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba mwaka 2021.

Mayala alisema kuwa mgawanyo wa dawa hizo ulikuwa, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe walipokea dawa zenye thamani ya Sh. milioni 11,359,400 na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ikiwa ni Sh. milioni 9.5. Akipokea dawa hizo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri Dk. Yahaya Msuya aliipongeza TMDA kwa kazi kubwa ya kudhibiti bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi iliyopelekea kukamatwa kwa dawa hizo.

Hata hivyo Dk. Msuya aliomba TMDA kuongeza kasi katika kuimarisha ukaguzi kwenye vituo binafsi vya kutolea huduma za afya kwa mikoa ya Mbeya na Songwe kwa madai kuwa ni maeneo yanayopakana na nchi mbalimbali.

"Vituo binafsi hasa maduka ya dawa muhimu kwa sasa ndio mahali pa kwanza ambapo jamii inakimbilia kupata huduma, kuna vitu vya ovyo sana vinafanyika katika vituo hivyo, kuna bidhaa ambazo zimeisha muda wake wa matumizi zisizosajiliwa na duni," alisema Dk. Msuya.

Aidha aliiomba mamlaka hiyo, kuongeza kiwango cha faini kitakacho sababisha watu wasirudie kufanya makosa kwa kuwa kiwango kinachotozwa kwa sasa kinasababisha watu warudie makosa wakijua watumudu kilipa," aliongeza Dk. Msuya.

Naye Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Sidney Mdoe, aliishukuru TMDA kwa kuwakumbuka katika mgawo wa dawa hizo zitakazosaidia katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyo mkoani Songwe.




Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Yahaya Msuya (kushoto), akipokea dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 20.8, kutoka kwa Mkaguzi Msaidizi wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Seleman Mayala, zilizotolewa na mamlaka hiyo juzi, baada ya kukamatwa zikiuzwa kinyume na sheria ya maduka ya dawa muhimu. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Serikali, wadau waombwa viwanda vya parachichi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZALISHAJI wa miche ya parachichi mkoani Mbeya, wamewaomba wadau na serikali kujenga viwanda vya kuongezea thamani zao la parachichi ili kuwasaidia kupata soko la uhakika kwa wakulima wanapozalisha.

Ombi hilo lilitolewa jana na wanakikundi cha parachichi kwanza kilichoko jijini Mbeya ambacho kinajishughulisha na uzalishaji miche ya zao hilo.

Mmoja wa wakulima, Janeth Mwamlima, alisema shughuli hiyo imewasaidia kumudu gharama za maisha kwa kila mmoja wao, hivyo uwapo wa viwanda kama vile vya kutengeneza mafuta ya kupakaa yatokanayo na parachichi utasaidia kuongeza mahitaji ya zao hilo sokoni hivyo wazalishaji nao watafaidika.

Alisema kuongezeka kwa mnyororo wa thamani wa zao hilo kwao itakuwa na manufaa makubwa kwa sababu mahitaji ya miche yatakuwa makubwa hivyo wataongeza kiwango cha kuzalisha.

James Pilla, alisema kuwa licha ya kuanzisha Kikundi cha Parachichi Kwanza mwaka 2021 na kutambuliwa na serikali ya Mkoa wa Mbeya, wameanza kupata zabuni mbalimbali kutoka kwa kampuni na wakulima wakihitaji miche ya kupanda.

Alisema licha ya kuanzisha kikundi hicho, lakini hawana maarifa ya kutosha kuhusu uzalishaji wa miche ya parachichi hivyo waliwaomba Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Uyole kuwapatia elimu ya kuzalisha kwa kuzingatia ubora.

"Baada ya kuanzisha kikundi chetu cha kuzalisha miche bado tulikuwa tunashindwa kuzalisha katika ubora unaotakiwa hivyo sisi waoteshaji tuliwaomba wataalamu wa kilimo kutoka TARI Uyole watupatie elimu ya kuandaa vitalu na kuotesha miche kwa kuzingatia kanuni za kilimo bora," alisema Pilla.

"Tuliamua kutembelea TARI, Uyole kwa lengo la kujifunza njia za kisasa za kuzalisha miche bora ya parachichi ukizingatia zao hili ni la kimkakati tumefundishwa mambo mengi ambayo yatasaidia kuzalisha kwa tija," aliongeza Pilla.

Alisema kuwa zao la parachichi limekuwa ni fursa kwa sababu limetoa ajira kuanzia wazalishaji wa miche na wakulima shambani pamoja na wanunuzi, wazalishaji, na kwamba wamejipanga vizuri kuongeza ujuzi wa namna bora ya kuzalisha miche ambayo itatoa matunda mazuri yatakayoweza kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

"Ni fursa kwa Mkoa wa Mbeya na nje ya nchi kulima zao la parachichi ambalo kwa sasa limekuwa dhahabu ya shambani sisi waoteshaji wa vitalu vya miche tunaendelea kuongeza maarifa ya namna bora ya kuzalisha miche ambayo itazalisha matunda yanayohitajika katika soko la kimataifa," alisema Pilla.

Alisema soko la miche linazidi kukua kila siku, na kwamba kabla ya kujiunga kwenye Kikundi cha Parachichi Kwanza alikuwa na uwezo wa kuzalisha miche 5000 hadi 7000 kulingana na mahitaji ya soko la dunia.

Alisema kikundi chao wanatarajia kuandaa kitalu na kuandaa miche kati ya 20,000 hadi 30,000 kwa mwaka 2022/2023.

Mtafiti wa zao la parachichi kutoka TARI Uyole, Daud Mbongo, alisema waliamua kukisaidia kikundi cha Parachichi Kwanza kuwapatia elimu ya uzalishaji bora wa miche ili waweze kuzalisha wa tija na kupata soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema walifikia uamuzi wa kukisaidia kikundi hicho baada ya kubaini mapungufu katika uzalishaji wa miche hiyo hivyo walianzisha darasa ya kuwafundisha mbinu mbalimbali za kuwawezesha kuzalisha kwa kuzingatia ubora unaotakiwa.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kituo hicho kinafanya utafiti wa mazao mbalimbali ikiwamo na matunda kama vile parachichi.

## Wanakijiji waliomba Bunge kupata zahanati

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WAKAZI wa Kijiji cha Majimoto Kata ya Nanyala, Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe wameomba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuwasaidia kupata zahanati ili waondokane na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu.

Waliyasema hayo juzi mbele ya kamati hiyo kwamba kijiji hicho hakina eneo la kutolea huduma za afya pamoja na shule ya msingi hivyo kusababisha adha ya kutumia umbali mrefu kwa watoto kwenda shule za mbali na wagonjwa kufuata huduma za matatibu maeneo mengine.

Alisema mara kadhaa hasa nyakati za masika watoto wamekuwa wakihangaika kuvuka mito na kuhatarisha usalama wao ili kwenda shule zilizoko vijiji vingine. Mmoja wa wakazi hao, Juma Mbwama, alisema ujio wa kamati kunaweza kusaidia kutatuliwa kwa vikwazo na kuiomba kamati, hivyo kuwataka wananchi wa Kijiji cha Majimoto kwa jicho la huruma.

"Licha ya uwapo wa shughuli za uendelezaji wa Jotoardhi yaani majimoto katika eneo hili wananchi tunahitaji kuona huduma mbalimbali za kijamii zikisogezwa karibu yetu mfano uwepo wa zahanati, shule za msingi na sekondari pamoja na kuboreshewa barabara kutoa eneo la mradi hadi kufika barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) yenye urefu kilomita 10," alisema Mbwama.

Alisema licha ya vikwazo vinavyowakabili lakini uendelezaji wa eneo hilo la chanzo cha majimoto umewapa faraja kutokana na upekee na historia ya eneo kwani wazee wa kijiji wamekuwa wakilitunza na kufanya matambiko hali iliyosaidia eneo hilo kutoharibiwa.

Naye Flora Baton alisema uwapo wa mradi umenufaisha vijana wa eneo hilo kwani baadhi yao wameweza kuajiriwa kwenye mradi huo kama walinzi, watunza mazingira na shughuli nyingine zinazoendelea kwenye mradi huo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dastan Kitandula, aliwasihi wananchi kuendelea kutunza mazingira ya eneo hilo la majimoto ili uoto huo uliopo uendelee kuwapo.

Kitandula alisema vikwazo vyote walivyovitoa kamati imevipokea na kwamba watazifanyia kazi kwa kuhakikisha mamlaka zinazohusika zinawafikia wananchi na kero hizo kutatuliwa.

Akizungumzia mradi huo, Mkurugenzi na Meneja mradi, Mhandisi Kato Kabaka, alisema eneo la majimoto lilipo Kata ya Nanyala wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe, wamekiteua kuwa kituo cha umahiri cha uendelezaji jotoardhi nchini.

Na alisema hadi sasa wameweza kutotolesha vifaranga kwa kutumia joto linalopatikana kwenye chanzo hicho cha majimoto.

## Watakiwa umakini matumizi ya vifaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIKUNDI vya wajasiriamali wa rasilimali za bahari za uvuvi, mwani, majongoo bahari wanaopatiwa mafunzo na Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, kutumia kwa utaratibu mzuri vifaa watakavyopewa ili viwe endelevu na kuleta tija kwao na vizazi vijavyo.

Waziri wa Wizara hiyo, Suleiman Masoud Makame, alitoa agizo hilo juzi wakati akizindua mafunzo kwa wajasiriamali hao yaliyofanyika Mkokotoni, mkoa wa Kaskazini Unguja.

Suleiman alisema serikali imetenga fedha nyingi kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kuwasaidia wajasiriamali hao kufanya kazi ili kuinua kipato chao na uchumi.

Alisema serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 36 kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vya wajasiriamali hali itakayosaidia kupunguza ukosefu wa ajira ndani ya jamii.

Suleiman aliesema vifaa hivyo vinajumuisha boti za uvuvi, boti za ukulima wa mwani, ufugaji wa samaki, majongoo bahari na kasa na vifaa vyake kwa kiasi kikubwa vitawafanya wajasiriamali kufanya kazi zao kwa ufanisi na kwa kiwango cha juu, hivyo kuwainua kiuchumi.

Kwa mantiki hiyo, alisema wajasiriamali hao hawana budi kuvitumia ipasavyo ili viwe endelevu kwa manufaa yao na vizazi vijavyo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, alisema mafunzo hayo ni moja ya hatua za serikali za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuitumia vyema rasilimali ya uchumi wa bluu kwa vile bado haijatumika ipasavyo. Takribani vikundi 436 vitafaidika na mikopo isiyo na riba ndani ya mkoa wa Kaskazini Unguja.

Naye Shabaan Hassan Ramadhani kutoka Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuachana na uvuvi haramu jambo ambalo husababisha kuathirika kwa mazingira ya bahari na rasilimali zake.

# SMZ yavalia njuga kero za elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa kushirikiana na wadau, imepanga kuzipatia ufumbuzi kero zilizoko katika sekta ya elimu ili jamii ipata huduma bora.

Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, aliyasema hayo jana kwenye ziara yake ya kutembelea sekta ya elimu katika maeneo ya mkoa wa Mjini Magharib zikiwamo shule za Mtopepo, Mwanakwerekwe na Bweleo katika wilaya ya Magharibi B.

Alisema kwamba uhaba wa madarasa ya kusomea, madawati, maabara na uwiano wa walimu na wanafunzi pamoja na nyenzo zingine za kujifunzia ni mambo ambayo serikali inafanya jitihada maalum kuhakikisha yanapatiwa ufumbuzi hatua kwa hatua.

Othman alisema kupitia miradi ya kupambana na UVIKO - 19, elimu ni miongoni mwa sekta zilizopatiwa fedha nyingi kuendeleza miradi ya ujenzi wa shule mpya pamoja na masuala muhimu yanayohusu miundombinu.

Pamoja na fedha hizo, alisema serikali itajitahidi kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha kunakuwa na matokeo chanya katika jitihada za kuimarisha utoaji wa huduma bora za elimu Zanzibar kwa vile ni sekta kiongozi katika jitihada za kuleta maendeleo. Pia aliishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kushirikiana na sekta mbalimbali zinazohusika na usimamizi wa ardhi kuwa na mipango endelevu ya kutenga ardhi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya elimu.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, alisema wizara hiyo inaendelea na utekelezaji wa programu na mipango katika kuhakikisha sekta ya elimu inaimarika.

Alisema miradi hiyo inajumuisha mapitio ya mitaala, ujenzi wa shule mpya zenye maabara za kisasa, ununuzi wa vifaa sambamba na kuzingatia uwiano wa wanafunzi na walimu darasani ili kuhakikisha huduma bora za elimu zinatolewa.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Mtopepo 'B', Bisihaba Hassan Chum, alisema shule hiyo ina matatizo kadhaa yakiwamo idadi kubwa ya wanafunzi darasani, uhaba wa vyoo, walimu pamoja na maabara mambo ambayo yanahitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka.




Mkurugenzi Mtendaji wa Chemba ya Biashara ya Zanzibar (ZNCC), Hamad Hamad (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Peak Performance International Tanzania, (PPIT), Philemoni Kisamo, wakisaini makubaliano ya kushirikiana kuendesha mafunzo ya aina mbalimbali ya kuendesha na kuleta mafanikio kwa wafanyakazi na wanachama wa Chemba hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wa (pili kushoto) ni Mwenyekiti wa ZNCC, Ali Amour. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rais Mwinyi asisitiza kasi upatikanaji wa maji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema lazima serikali iongeze kasi ya upatikanaji wa maji kwa wananchi kutokana na umuhimu wa huduma hiyo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la mradi mkubwa wa uhuishaji na uimarishaji wa mfumo wa majisafi na salama, Kwarara Kidutani, Wilaya ya Magharibi 'B', sambamba na maadhimisho ya Wiki ya Maji.

Alisema utekelezaji wa mradi huo uliowekwa jiwe la msingi ni katika kuyafikia malengo huku akisisitiza kwamba hatua hiyo ni ndani ya miaka miwili tu na hana shaka ndani ya miaka mitano ijayo tatizo la maji litamalizika.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, takwimu zinaonyesha kwamba hali ya upatikanaji wa maji kwa Zanzibar hivi sasa ni wastani wa asilimia 55 hadi kufikia mwaka huu na kwamba kukamilika kwa mradi huo, upatikanaji wa maji utafikia asilimia 76.

Rais Mwinyi alitoa wito kwa wizara husika na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kufanya kazi na kuwa wepesi wa kutatua changamoto za huduma hiyo zinazowakumba wananchi.

Alisisitiza kwamba jukumu la ulinzi la miundombinu ya maji ni la watu wote na kwamba wananchi wana jukumu la kuilinda miundombinu hiyo na wasiwaruhusu watu wachache kuiharibu.

Aidha, Dk. Mwinyi alisema upatikanaji wa huduma za majisafi na salama katika maeneo yote ya Unguja na Pemba ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika upatikanaji wa huduma za majisafi na salama ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, mipango mikuu ya maendeleo na ahadi zilizotolewa katika kipindi cha kampeni.

"Leo (juzi) tupo hapa Kwarara mkoa wa Mjini Magharibi kufungua ukurasa mwingine wa maendeleo ya sekta ya maji kwa kuweka jiwe la msingi la mradi mkubwa wa kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji katika maeneo mbalimbali ambapo huduma hii haipatikani kabisa", alisema.

Rais Mwinyi alisema mradi huo utanufaisha zaidi maeneo ambayo kwa sasa yanaonekana kukua kwa haraka kutokana na wananchi wengi kujenga makazi yao mapya na kuhamia maeneo hayo ya Wilaya ya Magharibi 'A' na Magharibi 'B' pamoja na maeneo ya mpakani mwa Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kusini Unguja yakiwamo Tunguu, Jumbi na Ubago.

Alisema maadhinisho hayo ambayo yanakwenda na kaulimbiu "Rasilimali za Maji Chini ya Ardhi ni Nyenzo ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi" na kusisitiza kuwa na mipango mbadala na mikakati itakayowezesha kukabiliana na changamoto za tabianchi.

Dk. Mwinyi alisema mabadiliko ya tabianchi ndiyo yanayosababisha uwezo wa uzalishaji wa maji katika vyanzo vilivyoko kupungua kama inavyoshuhudiwa katika vyanzo vya Mwanyanya na Mtopepo.

Alisisitiza kwamba katika hali kama hiyo ni lazima wananchi waendelee kupewa elimu ya kuvilinda na kuvitunza vyanzo vya maji kwa kuepuka ujenzi karibu na vyanzo hivyo na kuacha tabia ya ukataji wa miti na misitu pale vilipo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**TEGEMEZA AUCTION MART LIMITED**

**Kesi nambari 150/2021/kesi namba 07/2021 MM 118/2022**

**Tangazo la Mnada wa Hadhara**

Kwa Mamlaka tuliyopewa na Hakimu Mfawidhi Mahakama ya Mwanzo Kawe kutakuwa na Mnada wa Hadhara wa uuzaji wa spea za magari aina mbalimbali kama ifuatavyo:

| Aina ya Spea | Tarehe ya Mnada | Eneo mnada utakapofanyika |
|---|---|---|
| - Taa za magari<br>- oili injini<br>- Spea za magari ambazo ni mpya | 23/4/2022 | Mbezi Beach Saa 4 asubuhi – Tangi Bovu Kituo |

**Kwa mawasiliano zaidi piga Simu namba 0719 187 677**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**

**Unapojibu tafadhali taja:**
**Kumb.Na: MMC/LD/26860/30**
**Tarehe: 21.03.2022**

**YAH: MILIKI YA KIWANJA NA. 67 KITALU"C" KIHONDA LAND OFFICE NAMBA**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro anapenda kutoa taarifa juu ya Kiwanja Na.67 Kitalu 'C' kihonda hapo awali kilitolewa kwa ndugu Alex A. Kigoda kupitia barua ya toleo yenye Kumb.Na. MG/L/10064 iliyotolewa muda wa miaka 33 kuanzia tarehe 1/7/1993 kwa matumizi ya makazi.
Mnamo tarehe 23/7/1996 Ndugu Alex A. Kigoda alirejesha miliki hiyo serikalini na ndipo kiwanja hicho kikamilikishwa kwa ndugu Abdallah Mwambange ambaye ameendeleza kwa kujenga nyumba ya makazi toka alipomilikishwa mwaka 1996.
Aidha tunakusudia kumilikisha kiwanja hicho kwa Ndg Mwakiselu Abdalah Mwambage ambaye ni msimamizi wa mirathi ya ndugu Abdalah Mwambange
Hivyo mtu yeyote mwenye pingamizi au maslahi juu ya kiwanja hiki anatakiwa kutoa taarifa kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Morogoro S.L.P 587 Morogoro ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya barua hii.

K.N.Y MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

---

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF HOME AFFAIRS**
**IMMIGRATION DEPARTMENT**

## APPLICATION FOR CITIZENSHIP

**Telegrams: IMMIGRATION OFFICER,**
**TELEFAX: +255 28 2542104**
**TELEPHONE +255 28 2500585**

**THE REGIONAL IMMIGRATION officer**
**P.O.BOX 1711**
**MWANZA**
**DATE: 15/03/2022**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN**
**JAMES EDWARD TODD**
**P.O.BOX 1462.**
**MWANZA**



Whose photograph appears above, is applying for Tanzania citizenship to the Hon. Minister of Home Affairs. His current nationality is British and he is from England (Great Britain)
His current occupation is a Researcher and his address is P.O.BOX 1462, Mwanza. He is living in Tanzania since 2011.
Any person who know/has any reasons as to why citizenship should not be granted to him should send us a written and signed statement of fact to the commissioner General of Immigration services, P.O.BOX 1181-DODOMA.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANANIAS MICHAEL MWANGA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye **USAJILI NAMBA T956 AUY, CHASSIS NAMBA KZJ780018328.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**DAR/TAB/RB/94569/2022**

---

**SHERIA YA 10 MIRATHI G.N 1963 R.E 2019**

**Mirathi imefunguliwa katika Mahakama ya wilaya ya Shinyanga**

**Usimamizi Madhubuti wa Mali Namba 3 ya 2021**

**TIMOTH JOSEPH.............................Muombaji**

**kusimamia Mirathi ya**
**JOSEPH MABULA............ambaye ni Marehemu**

**Kwa ambao inaweza kumhusu**

Mwombaji aliyetajwa hapo juu ameteuliwa kusimamia mirathi ya marehemu Joseph Mabula Shauri.

Mtu yeyote mwenye Maslahi au Pingamizi anafahamishwa kuwa shauri hilo litasikilizwa tarehe 25/03/2022, hivyo anaombwa kuwasilisha hoja yake kabla ya tarehe hiyo vinginevyo shauri litaendelea kusikilizwa bila ya kuwepo pingamizi.

RESIDENT MAGISTRATE
SHINYANGA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DELINA GENERAL INTERPRISES LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 551 CUP – TOYOTA VITZ.** Chassis namba **SCP13-0038075.** Engine **2SZ-FE1297.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/111807/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**STEPHEN SOKOITEI SISYA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST YE**NYE USAJILI NAMBA **T763 DKS, CHASSIS NAMBA NCP605004341** na **ENGINE NAMBA 2NZ4455354.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/115783/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Morogoro**

**Kituo cha CHAMWINO**
**Mkoa Wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na 10....2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU IDDI AHMAD NG'OMBE WA MOROGORO-KASANGA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ZENA BAKARI CHITANDA**

**TANGAZO**

***(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 31/03 /2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 21/03/2022

Mwaka 2022
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO
MOROGORO
HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI.**
**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA.**
**Usimamizi wa mirathi Na 16 /2021.**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU YASSINI A. FERUZI WA DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MOHAMED YASSINI AZIZI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 04 mwezi 04 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 03 mwaka 2022.**

.......................................................
**HAKIMU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**

**SHAURI LA MADAI NA.41/2019**

**JOSEPH CHIVILE NA WENZAKE 7.....................WADAI**

**DHIDI YA**

**MAJALIWA MWAMAKULA................MJIBU MAOMBI 1**
**LUMONCONS COMPANY LTD...........MJIBU MAOMBI 2**

**KWA : MAJALIWA MWAMAKULA**
**POPOTE ULIPO**

**YAH : WITO**
***(Amri) ya 21r,35 (1) sura ya 33 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.***

Kwa kuwa Joseph Chivile na wenzake 7 wamefungua maombi ya kukaza hukumu kwa mfumo wa kukukamata kama mfungwa wa kimadai.
Hivyo unatakiwa kufika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya mnamo tarehe 24/03/2022 saa 02:30 asubuhi bila kukosa ili uoneshe sababu kwanini ukazaji huo wa hukumu usitekelezwe kama ilivyoombwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu,pamoja na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 18/03/2022.

HAKIMU MKAZI,
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI,
MBEYA.

---


# NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

SIKU 27 MASHAMBULIZI RUSSIA - UKRAINE;

# Russia yadai kuteka kitongoji Makariv



Raia wa Ukraine waliokimbia makazi yao wakiaga katika treni inayoelekea Poland, wakiwa mjini Lviv, Magharibi mwa Ukraine jana. **PICHA: AP**

**Kyiv,** UKRAINE

UMOJA wa Mataifa (UN), umesema takribani wakimbizi milioni 3.5 wengi wao wakiwa watoto wamekimbia nchini Ukraine, tangu Russia ilipoanza mashambulizi nchini humo, Februari 24.

Wizara ya Ulinzi ya Ukraine, imesema vikosi vyake vimedhibiti tena kitongoji muhimu cha Kyiv cha Makariv.

Mazungumzo ya upatanishi ya wajumbe wa Russia na Ukraine Jumatatu, wiki hii, yalidumu kwa saa moja na nusu, baada ya hapo majadiliano yaliendelea katika muundo wa kujigawa kwenye makundi, anasema mjumbe wa Ukraine na kiongozi wa wabunge wa cha chama tawala cha Ukraine Servant of the People, David Arahamiya.

Mazungumzo yalianza Februari 28, ilikuwa siku ya tano ya uvamizi wa majeshi ya Russia nchini Ukraine, wakati wawakilishi wa pande hizo mbili zinazozozana walikutana kwa mara ya kwanza huko Belarus, katika mkoa wa Gomel, kwenye mpaka wa Ukraine karibu na Mto Pripyat.

Ujumbe wa Russia, uliongozwa na mmoja wa wasaidizi wa karibu wa Rais Vladimir Putin, Vladimir Medinsky, Waziri wa zamani wa Utamaduni na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Historia ya Kijeshi ya Urusi.

Upande wa Ukraine uliongozwa na Waziri wa Ulinzi wa nchi hiyo Oleksiy Reznikov na mshauri mkuu wa ofisi ya rais Mykhailo Podolyak.

Awamu ya kwanza ya mazungumzo haikuzaa matunda yoyote. Na ilipofika Machi 1, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alisema yuko tayari kuzungumza moja kwa moja na Vladimir Putin. Lakini hakukuwa na hatua kubwa iliyopigwa.

**MALENGO YA MKUTANO**

Siku ya Jumatatu, Machi 21, mwaka huu, Ukraine na Russia, zilibadilishana tena taarifa juu ya mazungumzo ya ngazi ya juu.

Rais Zelensky amesema fursa pekee ya Rais Putin ya kuepuka maafa kwa Urusi ni kufanya mazungumzo ya amani.

Msemaji wa Kremlin, Peskov aliweka wazi kwamba ni mapema mno kuzungumzia uwezekano wa mkutano kati ya Putin na Zelensky, kwa sababu hawatakuwa na chochote cha kurekebisha, bado hakuna makubaliano.

Tangu kuanza kwa vita na tangu mwanzo wa mazungumzo ya kwanza, mambo mengi yamebadilika kwa pande zote kwa Ukraine na Russia. Mashambulizi ya mara kwa mara ya makombora na silaha yaliyofanywa na wanajeshi wa Russia, ikiwa ni pamoja na kuwalenga raia yalisababisha kuwapo kwa mamilioni kadhaa ya wakimbizi na raia wengi kujeruhiwa.

Licha ya ukweli kwamba mchakato wa mazungumzo, kulingana na wawakilishi wa Ukraine, ni mgumu, na kwa taarifa za kuvuja mara kwa mara za mazungumzo kutoka pande zote mbili kuna taarifa za matumaini, kwamba kuna fursa ya kufikia maelewano na baadhi ya mambo muhimu ya mkataba wa baadaye yanakaribia kukubaliwa.

> Russia, ilikuwa imeviambia vikosi vya Ukraine viondoke kwenye mji huo wa Pwani, kufikia saa 11 Alfajiri, siku ya Jumatatu wiki hii, saa za Moscow, lakini Kiev imesema hilo haliwezekani.

Volodymyr Zelenskyy katika moja ya mikutano ya waandishi wa habari alisema kuwa mazungumzo yalijaa maudhui kwamba: Wawakilishi wa Ukraine na Urusi wanajadili masuala fulani, walianza kuzungumza juu ya kitu fulani, na sio kutupa mahitaji ya ukomo.

Vladimir Putin, akimpokea Alexander Lukashenko huko Ikulu ya Kremlin, anasema kuwa mazungumzo hayo sasa yanafanyika karibu kila siku na kuna mabadiliko fulani mazuri.

**PANDE MBILI ZINAHITAJI NINI?**

Russia inataka Ukraine kukubali kwamba inapaswa kutoegemea upande wowote na haipaswi kuomba kujiunga na Nato. Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky tayari amekubali hilo.

Madai mengine ni kwamba Ukraine italazimika kupitia mchakato wa kuondoa silaha (mipakani) ili kuhakikisha kuwa si tishio kwa Russia. Lazima kulindwa kwa lugha ya Kirussia nchini Ukraine. Na kuna kitu kinachoitwa de-Nazification.

Mshauri na msemaji mkuu wa Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, Ibrahim Kalin akirejea mazungumzo yaliyosimamiwa na nchi yake alisema kwamba madai mengine ya Russia, yanahusisha hali ya Donbas, Mashariki mwa Ukraine, sehemu ambazo tayari zimejitenga na Ukraine na kusisitiza ni sehemu ya Russia, na hali ya Crimea.

Ingawa Kalin hakufafanua kwa undani zaidi, ila maelezo yake yanaleta dhana kwamba Russia itaitaka serikali ya Ukraine kuachia eneo mashariki

Ukraine yenyewe inataka kuwa huru, ijiamulie inavyotaka ikiwemo uwezekano wa kujiunga na Umoja wa Ulaya (EU).

Machi 16, Mwaka huu, Msemaji wa Vladimir Putin, Dmitry Peskov alithibitisha kuwa mazungumzo ya kusitisha mapigano kati ya Russia na Ukraine yaligusia kuhusu kuwa na Ukraine isiyoegemea upande wowote.

Hata hivyo, Katibu Mkuu wa NATO Jens Stoltenberg katika mahojiano na NBC, ingawa alishukuru Uturuki kwa juhudi zake za kuunga mkono mazungumzo ya Ukraine na Russia, lakini alibainisha: Ni mapema mno kusema kama mazungumzo haya yataleta matokeo yoyote thabiti."

Zelensky katika mahojiano na kituo cha televisheni cha Marekani CNN siku ya Jumapili anasema: "Nadhani tunahitaji kutumia njia yoyote, nafasi yoyote, ili kuwe na fursa ya mazungumzo, fursa ya kuzungumza na Putin. Lakini ikiwa majaribio haya yatashindwa, itamaanisha mwanzo wa Vita Kuu ya Tatu ya Dunia."

**HADI SASA:**

Ukraine imekataa agizo la Russia, kuwa vikosi vyake vijisalimishe na kuweka silaha chini kwenye mji wa Mariupol ambao umeendelea kushuhduia mashambulizi mazito.

Russia, ilikuwa imeviambia vikosi vya Ukraine viondoke kwenye mji huo wa Pwani, kufikia saa 11 Alfajiri, siku ya Jumatatu wiki hii, saa za Moscow, lakini Kiev imesema hilo haliwezekani.

Wizara ya Ulinzi ya Russia, ilidokeza kuwa, iwapo wanajeshi wa Ukraine wangejisalimisha, mipango ingewekwa ili kuwaruhusu watu kuondoka katika mji huo ambao kwa wiki kadhaa sasa umegeuka kuwa uwanja wa mapambano.

Wakati hayo yakijiri, Meya wa mji wa Chernigiv, Kaskazini mwa Ukraine ,amesema raia kadhaa wamepoteza maisha baada ya vikosi vya Russia, kushambulia hospitali moja.

Rais Zelensky akiwahutubia wabunge wa Israel ameendeleza wito wake wa mazungumzo na Russia ili kusitisha vita vinavyoendelea huku akisema mji wa Jerusalem, ni eneo sahihi la kuandaa mazungumzo hayo.

Wanajeshi wa Russia bado wanajaribu kuizingira Kyiv ambapo shambulio la bomu liliua takriban watu wanane usiku wa Jumapili hadi kuamkia Jumatatu.

Rais Zelensky amesema kuwa Ukraine haitakubali uamuzi wowote kutoka kwa Russia na kwamba maelewano yoyote yatabidi kwanza yakubaliwe na Waukraine kupitia kura ya maoni.

Baada ya mkutano wa Mawaziri wa Mambo ya Nje na Ulinzi wa Umoja wa Ulaya, Mkuu wa Sera ya Mambo ya Nje wa Umoja wa Ulaya, ametangaza kuhusu mkakati wa ulinzi wa umoja huo.

Hasa, ameelezea matakwa ya wanachama Ishirini na saba wa EU wa kuunda kikosi cha haraka cha kupeleka askari 5,000 au kuongeza sehemu ya matumizi ya kijeshi hadi asilimia mbili ya Pato la Taifa. Vikwazo vipya dhidi ya Russsia pia vimetangazwa.

Kulingana na msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya Russia, jeshi lake liko katikati mwa jiji la Mariupol ambapo lilipendekeza kwa mamlaka ya Ukraine kuweka chini silaha zao, bila mafanikio.

Russia, inadai kuwa imetumia makombora ya hypersonic tangu Ijumaa. Makombora haya yanaweza kuruka kwa karibu kilomita 12,000 kwa saa.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao.***

HABARI MICHEZO

# MTIFUANO LIGI KUU WANAWAKE ZANZIBAR KUENDELEA TENA LEO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Kuu ya Wanawake Zanzibar itaendelea leo katika viwanja vitatu tofauti ikiwa ni mzunguko wa nane wa ligi hiyo inayoshirikisha timu10 visiwani hapa.

Katika Uwanja wa Ziwani, vinara wa ligi hiyo, Warriors Queens wenye alama 21, watawakaribisha timu ya Mkoani kutokea Kisiwani Pemba, Mkoani ipo nafasi ya tano katika msimamo wa ligi ikiwa na alama 12.

Katika Uwanja wa Ngome timu ya Green Queens iliyopo nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 12, itaikaribisha timu ya Bungi Sisters kutoka Mkoa wa Kusini Unguja, inayoshika nafasi ya sita na alama zake tisa.

Mechi nyingine hii leo itapigwa Uwanja wa Bungi ambapo New Generation inayoshika nafasi ya pili ikiwa na alama 15 kwenye msimamo wa ligi hiyo, watavaana na vibonde, Dunga Queens wanaoburuza mkia kwa pointi zao mbili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Soka la Wanawake ZFF, Ali Ussi, alisema tangu kuanza kwa ligi hiyo, imeendeshwa kwa umakini kwani hawajapokea malalamiko yoyote rasmi hadi sasa licha ya kuwapo changamoto ndogo wakati huu ikiwa mzunguko wa nane.

Alisema kumekuwapo na changamoto kadhaa zinazojitokeza ikiwamo wachezaji kuwalalamikia waamuzi kutochezesha vizuri na kwamba Kamati ya Waamuzi imeanza kuifanyia kazi.

Ussi alisema ligi hiyo inatarajiwa kumaliza mzunguko wake wa kwanza mapema Machi 29, kwa kila timu kucheza michezo tisa na kwamba utaanza mapema Mei baada ya kumalizika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

KWISHINEI...



Pierre-Emerick Aubameyang (kushoto), akishangilia na kupongezwa na wachezaji wenzake wa Barcelona baada ya kuifungia bao la nne wakati ikishinda 4-0 dhidi ya Real Madrid kwenye mechi ya LaLiga iliyopigwa Uwanja wa Santiago Bernabeu mwishoni mwa wiki. **PICHA: MTANDAO**

## *Gofu Europe Tour kurindima Manyara*

**Saada Akida na Shuffa Lyimo**

CHAMA cha Mchezo wa Gofu Tanzania (TGU) kwa ushirikiano na serikali, kinatarajia kuwa wenyeji wa mashindano ya Gofu Europe Tour yatakayofanyika Juni 7 hadi 10, mwaka huu katika viwanja vya Kilimanjaro Gofu State, Manyara.

Mashindano hayo ni maalum kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za serikali inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza utalii wa Tanzania. Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa TGU, Chris Martin, alisema kwa Tanzania ni mara ya kwanza kuandaa mashindano hayo makubwa ambayo yatashirikisha mataifa mbalimbali.

Alisema wachezaji 136 wamethibitisha kushiriki mashindano hayo ambapo Tanzania imetoa wachezaji 10 huku nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Malawi kila moja ikitoa wachezaji wawili.

"Kwa ukanda wetu ni jumla ya wachezaji 10 na 126 ni kutoka bara la Ulaya, Asia na mataifa mengine, nina imani mashindano haya yatatoa fursa kwa kutangaza utalii wa Tanzania," alisema Mwenyekiti huyo.

Alisema TGU imeomba Tanzania kuandaa mashindano hayo ambayo mwaka jana yalifanyika Kenya na tunatarajia kwamba baada ya mwaka huu na mwakani, tutaanda kwa mara ya pili kuwa tena wenyeji.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Maendeleo ya Michezo nchini, Yusuph Singo, alisema ni jambo nzuri lakini serikali itakutana na Chama cha TGU.

"Kwa sasa hatuwezi kuzungumza lolote kwa sababu serikali tutapanga kukutana na kuzungumza na chama husika na baada ya hapo tutatoa tamko kuhusu uwenyeji wa mashindano hayo,"

# Namungo yafuata makali ya Ligi Zambia

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Namungo FC , kimeweka kambi ya wiki moja nchini Zambia kikijiandaa na michezo iliyobakia ya Ligi Kuu Tanzania Bara hususan unaofuta dhidi ya KMC FC baada ya Kalenda ya Fifa kumalizika mwishoni mwa wiki hii.

Namungo FC ambayo ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi 25, itakaporejea nchini, itakuwa ugenini Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kuvaana na KMC FC Aprili 3, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Namungo FC, Omary Kaaya, alisema kambi waliyoiweka nchini Zambia ni ya kimazoezi na wenyeji wao, Klabu ya Lusaka Dynamos.

**Alisema programu am bayo walipewa na benchi la ufundi linaloongozwa na Honor Janza, kambi hiyo itakuwa ya wiki moja kwa ajili ya maan dalizi ya michezo yao ili yobakia ya Ligi Kuu.**

"Kuhusu michezo ya kirafiki, hatujawa na ratiba hiyo kwa sababu tuna wasikiliza wenyeji wetu Lusaka Dynamos, kama itakuwapo tutaweka wazi," Kaaya alisema na kuongeza:

"Hiyo Kambi ni sehemu yetu ya maandalizi ya michezo iliyobaki ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, kuhakikisha tunafanya vizuri katika mechi zetu na kufikia malengo."

Alisema malengo ya kambi hiyo ni kupata sehemu tulivu kwa kipindi hiki cha Kalenda ya Fifa kwa ajili ya maandalizi yao hayo ili kuweza kufikia malengo tarajiwa.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DYBALA KUONDOKA JUVE
JUVENTUS imethibitisha kuwa Paulo Dybala ataondoka klabuni hapo msimu huu wa majira ya joto. Mshambulizi huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 28, aliwahi kutafutwa na Manchester United na Tottenham Hotspur. (***Fabrizio Romano)***

### OSIMHEN ATAKIWA NEWCASTLE
NEWCASTLE itarejea tena kampeni ya kumsaka mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen, licha ya klabu hiyo ya Italia kukataa ofa yake ya euro milioni 100 ya kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria Januari wakati dirisha la uhamisho lilipokuwa wazi. (***Express***)

### WANNE WATAJWA UNITED
MAURICIO Pochettino, Erik ten Hag, Julen Lopetegui na Luis Enriqueni ni miongoni mwa watu wanne wanaopigiwa upatu kuchukua usukani Manchester United huku klabu hiyo ikiendelea kumtafuta kocha atakayechukua nafasi ya Ralf Rangnick kwa mkataba wa kudumu msimu huu wa majira ya joto. (***Sky Sports***)

### MELO AWINDWA ARSENAL
ARSENAL wanajiandaa kumsajili Arthur Melo mwenye umri wa miaka 25, kutoka Juventus msimu huu wa majira ya joto baada ya kushindwa kufikia mkataba na kiungo huyo wa kati wa Brazil Januari. (***Calciomercato***)

### UNITED KWA RICHARLISON
MANCHESTER United wanamtaka mshambuliaji wa Everton na Brazil, Richarlison. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, pia amekuwa akihusishwa na Real Madrid, inayosimamiwa na kocha wa zamani wa Toffees hao, Carlo Ancelotti. (***Goal.com***)

### GAKPO AGOMBEWA ULAYA
KLABU za Ligi Kuu England, Arsenal na Liverpool wanamnyatia winga mahiri wa Uholanzi na PSV Eindhoven, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 22, lakini wanakabiliwa na ushindani mkali kutoka kwa Barcelona na Bayern Munich. (***Express via The Athletic***)

### POROZO AWANIWA CITY
MANCHESTER City wanajiandaa kuwasilisha dau la kumnunua mlinzi wa kati wa Boavista na Ecuador mwenye umri wa miaka 21, Jackson Porozo. (***Ojogo***)

### SAKA NA MKATABA ARSENAL
ARSENAL wana nia ya kumsainisha Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 20, mkataba mwingine wa muda mrefu. (***The Athletic***)

### LEEDS JICHO KWA CAKIR
KLABU ya Leeds United inamtaka golikipa wa Trabzonspor na Uturuki, Ugurcan Cakir mwenye umri wa miaka 25, na watamtazama katika mechi ya Alhamisi ya kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Ureno. (***Fanatik***)

### ADAMU LULU LEICESTER
KLABU ya Leicester City imejiunga na orodha ya klabu zinazotaka kumnunua mshambuliaji wa Salzburg na Austria, Chukwubuike Adamu mwenye umri wa miaka 20. (***Mail***)

### BARKAS ATAKA KUONDOKA
GOLIKIPA wa Celtic, Vasilis Barkas ameiambia klabu hiyo kwamba anataka kuhama msimu huu wa majira ya joto baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ugiriki mwenye umri wa miaka 27, kuwa kipa chaguo la tatu (***Daily Record, via Onlarissa)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# CAVANI KWENDA KUVAA VIATU VYA SANCHEZ INTER

●●● Barca nao wamehusishwa na taarifa za kuhitaji huduma ya straika huyo wa United, mwenye umri wa miaka...

**MILAN,** ITALIA

KLABU ya Inter Milan imevutiwa na mshambuliaji wa Klabu ya Manchester United, Edinson Cavani, ambaye mkataba wake na 'Mashetani Wekundu' hao unamaliza Juni mwaka huu kama mbadala wa Alexis Sanchez.Inter wanatafuta mashambuliaji ambaye anaweza kuongeza hamasa ya safu ya ushambuliaji kwenye timu hiyo, kwa sababu Sanchez anaweza kuruhusiwa kuondoka mwishoni mwa msimu.

**Cavani amefunga mabao mawili tu kwenye michezo 17 aliyoicheza Klabu ya Man United msimu huu.**

Majeraha yamekuwa kikwazo kwake msimu huu, huku msimu uliopita akifunga mabao 17 kwenye michezo 39 aliyocheza akiwa na jezi ya Mashetani Wekundu hao.

Barcelona nao wamehusishwa na taarifa za kuhitaji huduma ya mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 35, huku wakiwa na matumaini kuwa wanaweza kumshawishi kuweza kumwaga wino kwenye klabu hiyo.

Wachezaji wengine ambao wanahusishwa na klabu ya Inter ni Luis Suarez wa Atletico Madrid na Dries Mertens wa Napoli.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,065

MECHI KALI
POWER DYNAMOS
VERSUS
RED ARROWS
1 | 2.60
X | 2.60
2 | 3.03

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# RICHARLISON AWINDWA MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United wanataka kuimarisha eneo la ushambuliaji na wanavutiwa zaidi kumsajili mchezaji wa Brazil, Richarlson.

'Mashetani Wekundu' hao wamekuwa na uhaba wa mabao mengi msimu huu, ingawa wana wachezaji kama Jadon Sancho, lakini tatizo limekuwa eneo la mbele.

Richarlson ambaye anaichezea Everton ambao wanapambana kuepuka kushuka daraja msimu huu, ameifungia klabu hiyo mabao 42 kwenye Ligi Kuu England tangu aliposajiliwa mwaka 2018 kwa pauni milioni 35 akitokea Watford.

Kocha wa muda wa Man United, Ralf Rangnick anajiandaa kuachia nafasi hiyo mwishoni mwa msimu huu.

Na aliwahi kusema kwamba, klabu hiyo inahitaji kupata mshambuliaji mwingine kwa sababu mkataba wa Edinson Cavani unaelekea mwisho na Cristiano Ronaldo anaelekea ukingoni mwa kipindi chake cha uchezaji.

Carlo Ancelotti kocha wa Real Madrid pia aliwahi kuhusishwa kuitaka huduma ya Mbrazil huyo ambaye aliwahi kufanya naye kazi wakati akiinoa Everton kabla ya kuajiriwa na 'Los Blancos' hao.



# Chelsea na vita ya tiketi

**LONDON,** England

MASHABIKI wa Chelsea hawapaswi kuadhibiwa na vikwazo vya mmiliki wa klabu hiyo na wanatakiwa kuruhusiwa kununua tiketi za mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Crystal Palace mwezi ujao, kwa mujibu wa Mbunge wa Bunge la Uingereza, Julian Knight.

Chelsea inaendeshwa kwa vibali maalum kutokana na Serikali ya Uingereza kuiwekea vikwazo klabu hiyo na mali zote ambazo zinamilikiwa na bilionea Roman Abramovich ambaye anahusishwa kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na Rais wa Urusi, Vladimir Putin.

Kibali kilichotolewa na serikali hiyo kinairuhusu klabu hiyo kumalizia michezo yake na kulipa mishahara ya waajiriwa wake, lakini kinazuia kuuza tiketi na kufanya biashara yoyote, tiketi zinaweza kuuzwa ikiwa kibali chao kutafanyiwa marekebisho.

"Ni ajabu sana kutarajia kuona nusu uwanja kwenye Uwanja wa Wembley kwenye mchezo wa nusu fainali ya FA kati ya Chelsea na Palace," alisema Knight, ambaye ni Mw nyekiti wa Kamati ya M chezo, Sanaa na Hab wa Bunge la Uingereza.

"The Blues ni zaidi mmiliki, ni taasisi inay shi ikiwa na umuhim mkubwa kwa mashab na jamii, ilieleweka kwa ba ni notisi ya muda m pi, mchezo wa mwis dhidi ya Middlesbrou ulichezwa bila mashab wa Chelsea.

"Lakini kwa notisi FA hawana cha kujitet inabidi waruhusu kuuz kwa tiketi kwa mashab wa Chelsea ilimradi fed zitakwenda kwa watu Ukraine."

5,872,000

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/03/2022 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Cambridge Utd | 2.29 | 3.29 | 2.95 |
| 02. 26/03/2022 | 18:00 | Airdrieonians vs Cove Rangers | 2.73 | 3.27 | 2.42 |
| 03. 26/03/2022 | 18:00 | Elgin City vs Edinburgh City | 2.42 | 3.20 | 2.67 |
| 04. 26/03/2022 | 18:00 | Peterhead vs Falkirk FC | 2.78 | 3.32 | 2.35 |
| 05. 26/03/2022 | 18:00 | Leyton Orient vs Barrow | 2.24 | 3.29 | 3.04 |
| 06. 26/03/2022 | 18:00 | Carlisle vs Bristol Rovers | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 07. 26/03/2022 | 18:00 | Colchester vs Tranmere | 2.40 | 3.28 | 2.79 |
| 08. 26/03/2022 | 18:00 | Bradford City vs Newport | 2.56 | 3.20 | 2.66 |
| 09. 26/03/2022 | 18:30 | Den Bosch vs VVV Venlo | 2.36 | 3.72 | 2.55 |
| 10. 26/03/2022 | 19:00 | Finland vs Iceland | 2.28 | 3.15 | 3.30 |
| 11. 27/03/2022 | 15:00 | Mirandes vs Ponferradina | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 12. 27/03/2022 | 17:00 | Burgos vs Tenerife | 3.05 | 3.00 | 2.39 |
| 13. 27/03/2022 | 19:15 | Malaga vs Huesca | 2.49 | 3.08 | 2.83 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 23/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1378 | Alshoulla vs Al Khaleej Club | 2.45 | 2.89 | 2.89 |
| 16:00 | 2039 | Prison Leopards vs Indeni FC | 2.07 | 2.79 | 3.85 |
| 16:00 | 2788 | Green Eagles vs Zesco United | 2.65 | 2.65 | 2.89 |
| 16:00 | 2923 | Konkola Blades vs Kansanshi Dynamos | 2.80 | 2.51 | 2.90 |
| 16:00 | 4319 | Levadiakos vs Kallithea FC | 1.51 | 3.67 | 5.98 |
| 16:00 | 5326 | Power Dynamos vs Red Arrows | 2.60 | 2.60 | 3.03 |
| 16:15 | 2471 | Bisha FC vs Jeddah Club | 3.18 | 2.98 | 2.22 |
| 16:30 | 3758 | CR Belouizdad vs MC Alger | 1.99 | 2.92 | 3.93 |
| 16:30 | 5787 | Avellino vs Catania | 1.82 | 3.42 | 4.36 |
| 17:00 | 1651 | FK Zeleznicar Pancevo vs FK Loznica | 1.48 | 3.76 | 6.37 |
| 17:00 | 1892 | FK Buducnost Dobanovci vs FC Rad | 2.09 | 3.04 | 3.42 |
| 17:00 | 3083 | FK Zlatibor vs Macva Sabac | 1.95 | 2.99 | 3.96 |
| 17:00 | 3558 | Potenza SC vs Paganese | 2.10 | 3.22 | 3.52 |
| 17:00 | 4323 | FK Imt Novi Beograd vs Indjija | 2.79 | 2.70 | 2.70 |
| 17:00 | 4425 | FK Kabel Novi Sad vs FK Radnicki Sremska Mitrovica | 8.65 | 3.75 | 1.39 |
| 17:00 | 5978 | FK Timok 1919 Zajecar vs FK Zarkovo | 2.46 | 3.04 | 2.75 |
| 17:30 | 2262 | Tenisca vs UD Gran Tarajal | 1.90 | 3.45 | 4.10 |
| 17:30 | 5645 | CD Union Sur Yaiza vs CD Atletico Paso | 3.04 | 2.94 | 2.32 |
| 18:35 | 1246 | AL Adalh vs Hajer Club | 2.39 | 2.80 | 3.09 |
| 19:00 | 2199 | CD La Cuadra vs Lanzarote | 2.12 | 2.90 | 3.53 |
| 20:00 | 1751 | CD Marino vs Arucas CF | 1.87 | 3.27 | 3.84 |
| 20:30 | 4264 | Union Viera CF vs CD Santa Ursula | 2.61 | 2.94 | 2.65 |
| 20:45 | 2872 | Juventus Women vs Lyon W | 8.28 | 5.97 | 1.23 |
| 21:00 | 5282 | Vera Cruz PE vs Ibis PE | 1.77 | 3.66 | 3.81 |
| 21:05 | 3017 | Club Almagro vs Defensores Belgrano | 1.74 | 3.13 | 4.82 |
| 21:30 | 2804 | FC Gutersloh vs SG Wattenscheid | 1.97 | 3.96 | 2.94 |
| 21:30 | 3032 | Ratingen SV vs 1.fc Monheim | 1.78 | 4.05 | 3.42 |
| 21:30 | 3182 | Wacker Innsbruck II vs Telfs | 2.52 | 3.44 | 2.42 |
| 21:30 | 3813 | TSG Sprockhovel vs SPVGG Vreden 1921 | 1.47 | 4.54 | 5.03 |
| 21:30 | 4112 | Nova Iguacu RJ vs Audax Rio EC RJ | 2.26 | 2.90 | 3.19 |
| 21:30 | 5497 | ROT Weiss Ahlen vs RW Essen | 6.75 | 4.63 | 1.36 |
| 22:00 | 1399 | Deportivo Madryn vs Guillermo Brown | 1.93 | 3.09 | 3.86 |
| 22:00 | 1841 | Serc MS vs Aquidauanense MS | 2.27 | 3.04 | 3.04 |
| 22:00 | 2860 | SC Union Nettetal vs 1 FC Kleve | 6.77 | 5.22 | 1.31 |
| 22:00 | 3144 | Manchester City W vs Everton W | 1.11 | 7.55 | 14.51 |
| 22:00 | 3385 | Club Cortulua vs Envigado FC | 2.22 | 3.04 | 3.13 |
| 22:00 | 3581 | De Treffers vs VV Noordwijk | 2.26 | 3.57 | 2.65 |
| 22:00 | 3834 | Koninklijke Hfc vs Excelsior Maassluis | 1.72 | 3.86 | 3.86 |
| 22:00 | 4192 | Atletico Alvarado vs Brown Adrogue | 2.14 | 2.94 | 3.42 |
| 22:00 | 4613 | Deportivo Riestra vs Gimnasia Mendoza | 2.50 | 2.83 | 2.88 |
| 22:00 | 4937 | Deportivo Maipu vs Tristan Suarez | 2.36 | 2.70 | 3.27 |
| 22:00 | 5610 | SpVgg Sterkrade-Nord vs SF Niederwenigern | 2.02 | 4.04 | 2.79 |
| 22:30 | 1236 | Olivenza CF vs CD Don Alvaro | 1.63 | 3.51 | 5.00 |
| 22:30 | 4377 | CSD Arzua vs Silva SD | 2.15 | 3.08 | 3.22 |
| 22:30 | 5789 | Ourense CF vs SD Sofan | 1.21 | 5.37 | 11.52 |
| 22:45 | 1675 | Chelsea W vs Tottenham W | 1.08 | 7.92 | 20.28 |
| 22:45 | 4222 | Kingstonian vs Bowers Pitsea | 2.09 | 3.56 | 2.93 |
| 22:45 | 5912 | Truro City vs Yate Town | 2.40 | 3.42 | 2.56 |
| 23:00 | 3852 | Arsenal W vs Wolfsburg W | 2.50 | 3.32 | 2.50 |
| 23:05 | 1012 | Nueva Chicago vs San Martin Tucuman | 3.97 | 2.95 | 1.96 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# HOMEBOYZ YAMZUIA MWALALA KUTUA KUINOA COASTAL

**Na Cheji Bakari,** Tanga

MCHAKATO wa Klabu ya Coastal Union kuipata huduma ya Mkenya Bernard Mwalala kama kocha mkuu wa timu hiyo, umekwama na sasa kamati tatu zilizokuwa zinashughulikia suala hilo, zinakuna kichwa kupata mwalimu mwingine, imeelezwa.

Juhudi za kamati hizo, zimegonga ukuta kutokana na viongozi wa Klabu ya Kakamega Homeboyz ya Kenya, anayoinoa Mwalala kukataa kuvunja mkataba na kocha huyo kwa sasa huku ikimtaka asubiri hadi mwishoni mwa msimu.

Coastal Union ilikuwa ikimsaka Mwalala, ambaye aliwahi kuichezea timu hiyo pamoja na Yanga kwa nyakati tofauti, ili kuja kuchukua mikoba ya Melis Medo, aliyeachia ngazi hivi karibuni na kuiachia timu hiyo ikiwa chini ya msaidizi wake, Joseph Lazaro.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa Coastal Union, Salim Bawazir, akizungumza na mwandishi wetu kuhusu mchakato wao wa kumtaka Mwalala kuwa kocha mkuu, alisema suala hilo limeshindikana na sasa wanaangalia kwingineko.

"Ni kweli tulikuwa na mpango wa kumchukua Ben Mwalala kuwa kocha mkuu wa Coastal Union, ili asaidiane na Joseph Lazaro, na yeye



# *Makata aibukia Mbeya Kwanza*

**Na Adam Fungamwago**

BAADA ya kutimuliwa kazi kwenye kikosi cha Dodoma Jiji mwishoni mwa mwezi uliopita, Mbwana Makata ameibukia Klabu ya Mbeya Kwanza, akikabidhiwa kushika mikoba ya timu hiyo badala ya Maka Mwalwisi ambaye amerejeshwa kwenye kazi yake ya awali ya Ukurugenzi wa Ufundi.

Meneja wa timu hiyo, Davis Naftari amesema tayari Makata ametua ndani ya timu hiyo na alikuwa na mkutano na wachezaji, kabla ya kuanza kazi rasmi.

"Ni kweli Kocha Mbwana Makata tunaye, na kuna taarifa zinaenezwa kuwa Kocha Maka Mwalwisi amefukuzwa, hilo si kweli, ila yeye alikuwa anakaimu nafasi ya ukocha baada ya makocha kutimuliwa, kwa hiyo sasa tumepata kocha, yeye amerudi kwenye nafasi yake ya awali," alisema meneja huyo ambaye ni beki wa zamani wa Simba.

Alisema ujio wa kocha huyo unaweza kuwa mkombozi kwa timu hiyo kwa sababu morali ya wachezaji ilishuka.

"Wachezaji walipoteza kujiamini, walikuwa hawana morali, kusema kweli haikuwa kwenye mazingira mazuri, nashukuru alivyokuja amekaa kikao na wachezaji na wameonyesha kuwa sasa wana ari, ninaamini mechi ijayo au zinazofuata tutapata ushindi," alisema meneja huyo.


Kwa sasa Mbeya Kwanza ambayo imehamishia mechi zake za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Majimaji Songea, iko kwenye nafasi ya 15, ikiwa na pointi 14 kwa michezo 18 iliyocheza.

Makata alitimuliwa Dodoma Jiji FC, mwishoni mwa Februari, baada ya timu hiyo kutofanya vema kwenye mechi za Ligi Kuu.

# Michezo

Jumatano Machi 23, 2022

Nipashe

Richarlison awindwa United

UKURASA 22

HIYO...



Wachezaji wa Taifa Stars, Feisal Salum 'Fei Toto' (kulia) na Dickson Job wakiwa mazoezini juzi kujiandaa na mechi ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati itakayopigwa leo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: TFF**

## Stars, Afrika ya Kati vitani kwa Mkapa

**Na Saada Akida**

WAKATI timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars ikishuka dimbani leo kukabiliana na Jamhuri ya Afrika ya Kati katika mchezo wa kirafiki uliopo kwenye Kalenda ya Fifa, utakaopigwa Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam kuanzia saa 1:00 usiku, Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Kim Poulsen amewaita mashabiki kushuhudia burudani.

Taifa Stars itautumia mchezo huo kama sehemu ya maandalizi ya kujiandaa na michuano ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika zijazo (Afcon), inayotarajiwa kuanza Julai, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana katika Makao Makuu ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Poulsen, alisema maandalizi yameenda vizuri na wachezaji wanaocheza soka la kulipwa tayari wameungana na wenzao kambini.

Aliwataja wachezaji wanaocheza soka la kulipwa ambao tayari wameingia kambini kuwa ni Haji Mnoga (Weymouth - England) na Ben Starkie (Spalding United - England), Novatues Dismas (Beitar Tel Aviv Bat Yam - Israel) na Ibrahim Joshua (Tusker - Kenya).

"Kuhusu Mbwana Samatta na Kevin John (wanaocheza soka la kulipwa Ubelgeji) na wachezaji wa Simba wanaingia mchana wa leo (jana) na kuungana na wenzake kambini tayari kwa ajili ya mchezo huo.

"Hizi mechi ni muhimu sana kwetu kwa sababu zinatusaidia katika maandalizi ya timu kuelekea michuano ya AFCON na CHAN. Afrika ya Kati ni timu nzuri na ina wachezaji wazoefu na michuano mikubwa."

"Hii ni timu ya Watanzania, wote tunapigania taifa hakuna kuangalia timu, tuungane wote kusapoti Taifa Stars, sio kwa ajili ya timu fulani," alisema Kocha Poulsen.

# Simba: Subirini mtafurahi tu

## Wachezaji waangukia mashabiki, watoa ahadi nzito wakiitupia jicho Gendarmerie, wasema...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU wakiomba radhi kwa kupoteza mechi yao ya tano ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika na kushindwa kuweka rekodi ya kufuzu wakiwa ugenini, wawakilishi pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba, wamewatuliza mashabiki wao kwa kuahidi kuwafurahisha nyumbani dhidi ya US Gendarmerie.

**Simba imetua nchini jana ikitokea Benin ambapo ilipoteza kwa mabao 3-0 dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, hivyo kujikuta ikishika nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba sawa na RS Berkane ya Morocco huku Waivory Coast hao wakikaa kileleni mwa msimamo wa Kundi D wakiwa na alama zao tisa wakati US Gendarmerie yenye pointi tano ikiburuza mkia.**

Akizungumza na mwandishi wetu baada ya kikosi hicho kutua Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam jana, Nahodha wa Simba, Jonh Bocco, alisema wao kama wachezaji wana kila sababu ya kuomba radhi kwa viongozi na mashabiki wa timu hiyo kutokana na matokeo hayo ambayo hawakuyategemea.

Alisema hali kama hiyo hutokea na wakati mwingine timu bora uwanjani hupoteza mechi kitu ambacho watakahikisha hakijirudii katika mchezo ujao.

"Nichukue fursa hii kuwaomba radhi mashabiki, viongozi na Wanasimba wote kwa matokeo mabaya tuliyopata, sasa tunajipanga kwa mechi yetu ya mwisho nyumbani, ninaamini tutawapa furaha, kwani lengo letu ni kuingia robo fainali.

"Matokeo haya yametuumiza pia sisi wachezaji, lakini tumeyasahau na tunajipanga kwa mchezo wa mwisho dhidi ya US Gendarmerie," alisema Bocco.

Simba itaikaribisha US Gendarmerie katika mchezo wao wa mwisho wa Kundi D utakaopigwa Aprili 3, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na ushindi wowote kwenye mechi hiyo, utaiwezesha kufuzu hatua ya robo fainali.

Mechi nyingine ya Kundi D siku hiyo, itawakutanisha vinara wa kundi hilo, Asec Mimosas watakaokuwa ugenini nchini Morocco dhidi ya RS Berkane, ambao watahitaji kushinda ili kusonga mbele huku wageni zao sare yoyote ikiwapa tiketi ya robo fainali.

Kwa upande wa Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alisema waliondoka nchini kwenda Benin wakiwa na lengo la kuweka rekodi ya kufuzu ugenini, lakini hilo limeshindikana ila watatumia vema uwanja wa nyumbani wa Benjamin Mkapa kufuzu.

Alisema wanahitaji ushindi wowote katika mechi hiyo ya mwisho ili kufuzu bila kutegemea matokeo ya timu nyingine kwenye kundi hilo, hivyo hawatafanya makosa katika mchezo huo dhidi ya US Gendarmerie.

"Tumepoteza mchezo lakini hatujapoteza lengo letu la kutinga robo fainali, tulipanga kufuzu tukiwa ugenini ili kuweka historia, lakini imeshindikana, tumerudi nyumbani kujipanga kwa mchezo wa mwisho.

"Tiketi yetu ya kuingia robo fainali tunayo wenyewe, tunahitaji kushinda tu mchezo wetu bila kuangalia matokeo mengine ndiyo maana nasisitiza mashabiki kujitokeza kwa wingi Aprili 3 kwa Mkapa kuisapoti timu," alisema.

Baada ya kuwasili wachezaji wa Simba walioitwa timu zao za taifa wameruhusiwa kwenda kujiunga nazo na wale ambao hakuitwa wamepewa mapumziko mafupi kabla ya wote kurejea kambini Jumapili wiki hii, kujiandaa na mechi dhidi ya US Gendarmerie.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >